# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA SITA

### Kikao cha Tisa – Tarehe 6 Septemba, 2024

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

### D U A

*Naibu Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu.

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:**

### MASWALI NA MAJIBU

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali. Tunaanza maswali na Ofisi ya Waziri Mkuu. Mheshimiwa Amina Ali Mzee.

Na. 136

### Kupunguza Wimbi la Vijana Wanaomaliza Masomo na Kukosa Kazi

**MHE. AMINA ALI MZEE** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kupunguza wimbi la vijana wanaomaliza masomo na kukosa kazi kutokana na sharti la vigezo vya uzoefu wa miaka miwili na zaidi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Amina Ali Mzee, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuwezesha vijana wahitimu wa ngazi mbalimbali za elimu kuwa na uzoefu wa kazi pamoja na sifa nyingine za kujiajiri ndani na nje ya nchi, Serikali inaendelea na programu mbalimbali za mafunzo ya uzoefu wa kazi ikiwemo *internship* na maboresho ya Sera ya Taifa ya Vijana ya mwaka 2007 ambayo inahimiza uwepo wa mfumo endelevu wa kuwajengea vijana ujuzi na stadi mbalimbali ili waweze kuajirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia Bunge lako Tukufu ninaomba kutoa wito kwa wahitimu kutumia fursa zinazotolewa na Serikali kupitia programu za elimu, mafunzo na uwezeshaji wa kiuchumi kwa kutoa mikopo na mitaji, fursa za ajira rasmi na zisizo rasmi katika miradi ya Serikali inayopatikana katika Wizara za Kisekta na Sekta Binafsi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Amina.

**MHE. AMINA ALI MZEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa majibu mazuri ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia maboresho ya Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana, ni upi mkakati wa Serikali kuongeza ajira kwa vijana nchini? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia maboresho yaliyofanyika ya Sera ya Maendeleo ya Vijana, katika moja ya kitu kikubwa ambacho kimefanyika, kwanza ni kutambua vijana wenyewe ni akina nani.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kutambua vijana katika kila eneo la sekta ya kuzalisha ya kiuchumi na kimaendeleo kwa nchi yetu. Katika kufanya hivyo pia ndani ya Sera ya Vijana, moja ya kitu kikubwa ambacho kimeongezwa sasa chini ya uongozi wa Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, ni kuhakikisha kwamba tunakuwa na programu za malezi ili kumsaidia kijana huyu siyo tu ajiandae kuajiriwa ndani ya Serikali, lakini pia kumuwezesha hata kiuchumi, kifedha ili aweze kujiajiri mwenyewe na kuweza kujitegemea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ndani ya sera hiyo yapo maboresho makubwa mengi yaliyofanyika, lakini kubwa kuliko lote ni lile sasa la kutambua vijana katika kila sekta ya kimaendeleo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Janejelly.

**MHE. JANEJELLY J. NTATE:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na juhudi nzuri sana za Serikali kwa jinsi mnavyowaangalia vijana, je, sasa Serikali hamjaona kuna umuhimu wa kuchukua vijana kwa taaluma zao, kuwapanga pamoja na kutumia mikopo ya halmashauri mkisaidiana na TAMISEMI ili kuwapa hiyo mikopo waitumie kujiendeleza kitaaluma bila kutegemea ajira za Serikali? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo yaliyotolewa na Mheshimiwa Mbunge kwanza ninakiri kuyachukua kama ni ushauri mzuri, lakini ninataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali imeendelea kuhakikisha kwamba vijana wanawezeshwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya jambo kubwa inalofanya ni kuwawezesha vijana katika ujuzi ambapo programu mbalimbali ikiwemo Programu ya Uanagenzi nayo ni moja katika jambo kubwa ambalo linafanyika ndani ya Serikali ili kuwawezesha vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako kwamba Serikali itaendelea kuyafanyia kazi kuhakikisha kwamba tunawezesha vijana kwa sababu ukiwezesha vijana ndiyo umewezesha nguvu ya Taifa. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, kuna mradi Bangladesh wamezindua unaitwa *Decentralization and Eligible Energy*. Mradi huu unasaidia vijana wengi kuingia katika biashara hii, kupeleka umeme huu wa nishati ya jua kwenye vijiji vingi na wengi walijipatia ajira. Nendeni Bangladesh mkajifunze muone namna gani mtasaidia vijana wa Kitanzania. *(Makofi)*

Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Askofu Gwajima.

Na. 137

**Kuchonga Barabara za Vumbi – Kawe**

**MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha barabara za vumbi za Jimbo la Kawe zilizoharibiwa na mvua zinazoendelea kunyesha zinachongwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imechukua hatua za haraka kukabiliana na uharibifu mkubwa uliosababishwa na mvua kubwa iliyonyesha hivi karibuni katika barabara za udongo za Jimbo la Kawe.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuhakikisha usalama na ufikikaji wa barabara hizi muhimu za usafiri, Serikali imefanya matengenezo ya barabara za Jimbo la Kawe kwa kuchonga baadhi ya barabara hizo ambazo zimeathiriwa na mvua. Jumla

ya kilometa 66.32 za barabara tayari zimechongwa ambapo gharama zilizotumika mpaka sasa ni shilingi milioni 136.68.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea na kazi za ukarabati wa barabara zote zilizoathirika na mvua ili kuzirejesha katika hali yake ya awali kulingana na upatikanaji wa fedha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Askofu Gwajima.

**MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, ninalo swali moja dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Kawe lina mashina zaidi ya 1,000 na takribani kila shina lina barabara sita na huu ni mzigo mkubwa. Serikali ikitumia utaratibu wa kawaida inaweza isiweze kumaliza mzigo wa barabara hizi.

Je, Serikali ina mpango gani wa ziada wa kumaliza Barabara hizi ambazo ni karibu elfu sita na kitu? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nianze kwanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Mbunge, kwa kweli tunamwona jinsi gani anavyotembelea maeneo mbalimbali kutazama na kuleta msukumo katika kuhakikisha wananchi wake wanapata barabara zilizo bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, pamoja na kwamba Serikali inatenga fedha katika Manispaa ya Kinondoni shilingi bilioni saba kila mwaka kwa ajili ya kuhudumia barabara hizi za *TARURA,* lakini pia Manispaa ya Kinondoni ipo katika Mradi wa *DMDP II* ambao ni mradi wa jumla ya USD milioni 438. Mradi huu utaenda kusaidia sana katika kurekebisha barabara katika jimbo lako.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimtaarifu Mheshimiwa Mbunge na nimpongeze kwa sababu ninyi mkiwa kama sehemu ya Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni mmeweza kununua mitambo kupitia mapato ya ndani; mmenunua *wheel loader, grader* na *excavator* ambazo sasa hivi zipo katika hatua ya *clearance* na wiki ijayo mitambo hii itakuwa imetoka. *(Makofi)*

Sasa ninawapongeza kwanza, lakini ninachukua nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI kumwagiza Mkurugenzi, mara tu mitambo hii itakapotoka iingie *site*, ifike katika Jimbo la Kawe, ianze kuchonga barabara ili wananchi waweze kupata barabara nzuri kabisa. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahante, ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri. Mheshimiwa Kisangi.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto zinazolikuta Jimbo la Kawe zinafanana kabisa na zile za Jimbo la Kigamboni, maeneo ya *Kisarawe II*, maeneo ya Kigogo ya Viwandani, Mwasonga, Tundwi Songani, Kimbiji na Mkundi katika Kata ya Pemba Mnazi, maeneo haya barabara zimeharibika kabisa na mvua.

Je, Serikali ina mpango gani sasa wa kurekebisha barabara hizo ili zikae vizuri na wananchi wa maeneo hayo waweze kupita vizuri? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa kupaza sauti yake ili kuhakikisha wananchi wanaweza kutengenezewa barabara hizi ambazo ni muhimu sana kiuchumi, lakini kijamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba niendelee kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali kila mwaka wa bajeti inatenga fedha kwa ajili ya kuhudumia barabara hizi za *TARURA* ikiwemo katika Jimbo la Kigamboni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna nafasi ya Mkurugenzi kutumia mapato ya ndani kwa ajili ya kuhakikisha na yeye anaweza kusimamia katika kurekebisha barabara hizi. Mheshimiwa Mbunge ule Mradi wa *DMDP II* ambao ni mradi wa jumla ya USD milioni 438 na wenyewe unaenda kunufaisha Manispaa ya Kigamboni.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hatua hii tayari kazi zilishatangazwa na tayari wakandarasi wameshapatikana, ipo katika hatua za mwisho kabisa za ununuzi na mikataba itasainiwa ili wakandarasi waingie *site* waanze sasa kurekebisha barabara. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Chaurembo, ajiandae Mheshimiwa Waitara na ajiandae Mheshimiwa Dkt. Pallangyo.

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa halmashauri nyingi sasa zimeonesha uwezo wa kununua mitambo kwa ajili ya kuchonga barabara, je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha vitengo maalumu vya *maintenance* katika halmashauri hizi? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Naibu Waziri, kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni mawazo mazuri sana ya Mheshimiwa Mbunge, tumeyapokea, tutayachakata na tutayafanyia kazi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Waitara, ajiandae Mheshimiwa Dkt. Pallangyo.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri wa TAMISEMI alifanya ziara katika Jimbo la Tarime Vijiji, Makao Makuu ya Halmashauri Nyamwaga na aliahidi ujenzi wa kilometa mbili pale Makao Makuu, ninapenda kujua kama ile ahadi bado ipo au imeyeyuka? Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nipokee alichokisema Mheshimiwa Mbunge na baada ya kipindi hiki cha maswali na majibu tutafanya ufuatiliaji ili kujua imefikia hatua gani, utekelezaji wa ujenzi wa hizi kilometa mbili zilizoahidiwa na Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Dkt. Pallangyo.

**MHE. DKT. JOHN J. PALLANGYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto ya barabara za vumbi iliyoko kule Jimboni Kawe inafanana sana na hali ilivyo jimboni kwangu ambapo barabara nyingi zinapanda mlimani, je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka kuongeza bajeti ili kuondoa hiyo changamoto? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge kwa kweli amekuwa akisemea sana mazingira ya jimbo lake na hasa kwa sababu ya mazingira ya kuwa katika milima. Kwa hiyo, ninaomba nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge, tayari tumekuwa tukiwasiliana mimi na wewe. Kwa hiyo, tutaendelea kuhakikisha tunatengeneza msukumo ili kuweza kupatikana bajeti ya kutosha ambayo itakuja uhudumia barabara katika jimbo lako. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava.

Na. 138

**Ujenzi wa Uzio katika Shule ya Wasichana Abdulrahim Busoka**

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga uzio katika Shule ya Wasichana ya Abdulrahim Busoka ya kidato cha tano na sita?

**NAIBU SPIKA:** Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2021/2022 mpaka 2023/2024, Serikali Kuu imepeleka shilingi milioni 166.4 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa saba na matundu ya vyoo nane katika Shule ya Wasichana ya Abdulrahim Busoka kwa wanafunzi wa kidato cha tano na sita.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2024/2025 Serikali kwa kushirikana na *Barrick Tanzania* itatoa kiasi cha shilingi milioni 227.2 kwa ajili ya kujenga bweni moja, madarasa matatu na matundu sita ya vyoo. Serikali inatambua umuhimu wa uzio kwa ajili ya ulinzi wa mali na wanafunzi wa bweni.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, kwa sasa kipaumbele cha Serikali kuu ni ujenzi wa miundombinu ya msingi inayowezesha kuongeza nafasi za udahili wa wanafunzi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Mnzava.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa majibu ya Naibu Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, shule hii iko barabarani kabisa, njia kuu ya kutoka Kahama kwenda Rwanda na watoto wanakuwa kwenye *risk* kubwa sana, je, pamoja na kujenga miundombinu ya madarasa, hamuoni kuwa uzio nacho ni kipaumbele?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa kumekuwa na matukio mengi ya watoto kuvamiwa na kuibiwa mali zao na wazazi kuwa na wasiwasi na usalama wa watoto wao, je, hamwoni kuwa kuna umuhimu sasa wa kutafuta fedha za dharura ili uzio uweze kujengwa? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika,

ninaomba nijibu maswali ya Mheshimiwa Mbunge yote mawili kwa pamoja; kwanza nianze kwa kumpongeza sana kwa jitihada zake za kuhakikisha kwamba watoto wanasoma katika mazingira yaliyo salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali Kuu kwa sasa kipaumbele chake ni kuhakikisha kwamba inajenga miundombinu ya msingi ambayo itawezesha kupokea na kuongeza udahili wa wanafunzi, lakini masuala ya usalama wa wanafunzi wanapokuwa shuleni pia ni ya muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninaomba nichukue nafasi hii kumwagiza Mkurugenzi, afanye tathmini katika shule aliyoitaja Mheshimiwa Mbunge ili aweze kuona mazingira na aweke katika mipango ya mapato ya ndani ya halmashauri na kutenga bajeti kwa ajili ya kwenda kuweka uzio katika eneo hilo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Chaya.

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Katika Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni tumejengewa shule ya wasichana ya mkoa inaitwa *Solya Girls Secondary School* na tayari tuna udahili wa watoto 288 wa kidato cha kwanza na kidato cha tano lakini shule ile haina uzio.

Je, ni nini mkakati wa Serikali wa kuhakikisha kwamba ili kuwalinda watoto wa kike wanajenga uzio? Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge anazungumzia maslahi mapana kabisa na hasa ya usalama kwa wanafunzi wetu katika shule hii mahsusi kabisa ya wasichana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimfahamishe Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari Serikali Kuu imeshatoa fedha shilingi 50,500,000 katika shule zote hizi za mikoa za wasichana za sayansi kwa ajili ya kujenga uzio. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ninaomba niendelee kutoa msisitizo kwa Wakurugenzi kupitia mapato ya ndani ya halmashauri na wenyewe waweze kutenga bajeti kwa ajili ya kuhakikisha wanaunga mkono jitihada za kuboresha miundombinu na kuimarisha usalama wa Watoto, hasa katika shule hizi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kigua.

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Kilindi tunayo shule ya wasichana inaitwa *Kilindi Girls* na ni kwamba eneo hilo ambalo ipo hii shule ni eneo ambalo linazungukwa *at least* na msitu. Sasa kwa usalama wa wasichana ni jambo muhimu sana, je, Mheshimiwa Naibu Waziri, uko tayari kulipokea hili na kulifanyia kazi? Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kuzungumzia masuala ya kuimarisha usalama wa wanafunzi wetu wanapokuwa shuleni. Ninaomba nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge, hili tumelipokea na tutafanya jitihada kwa sababu Serikali imeanza kujenga miundombinu hii kwa awamu. Awamu ya kwanza miundombinu hii ya shule imepatikana na ndiyo maana watoto wameweza kuanza kusoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kila awamu Serikali itakuwa inaleta fedha kwa ajili ya kuendelea kuboresha miundombinu iliyobakia. Kwa hiyo, nimelichukua jambo lako hili Mheshimiwa Mbunge kwa ajili ya kulifanyia kazi.

**NAIBU SPIKA:** Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Anton Albert Mwantona.

Na. 139

**Hitaji la *Transformer* Vijiji vya Mpindo na Isumba – Rungwe**

**MHE. SUMA I. FYANDOMO K.n.y. MHE. ANTON A. MWANTONA** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itaweka *transformer* kwenye Vijiji vya Mpindo, Kata ya Bulyaga na Isumba, Kata ya Kinyara ili wananchi wanufaike na Mradi wa *REA III* Awamu ya II?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa *REA* Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili unalenga kupeleka umeme katika vijiji 31 katika Jimbo la Rungwe. Hadi sasa, jumla ya vijiji 30 vimeunganishwa na umeme na kijiji kimoja kilichobaki ambacho kinaitwa Kyobo Juu kilichopo Kata ya Ikuti kazi inaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Vijiji vya Mpindo na Isumba vilivyopo Kata ya Bulyaga na Kinyara tayari vimeunganishiwa umeme na tayari *transformer* imefungwa tangu mwezi Mei, 2024. Kwa sasa kazi inayoendelea ni kuunganisha wateja wa awali katika vijiji hivyo ambapo jumla ya wateja 43 kati ya 44 tayari wameunganishiwa umeme, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Suma.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa majibu mazuri ya Serikali na naipongeza Serikali kwa namna ambavyo inafuatilia vizuri na kukamilisha matatizo na kero za umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilayani Kyela kuna shida za vijiji ambavyo havijafanikiwa kupata umeme wa *REA*. Sasa je, ni lini Serikali itakamilisha vijiji hivyo ambavyo vipo kwenye Wilaya ya Kyela pamoja na kule Wilaya ya Mbarali na Wilaya ya Mbeya Vijijini? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, vijiji ambavyo hivi vimebaki katika hizi wilaya ambazo amesema Mheshimiwa Mbunge, ni vijiji vichache na wakandarasi wapo *site*. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa tunasimamia kwa weledi mkubwa sana kwa sababu muda wa kumalizika huu mradi ulishafika, kwa hiyo, wakandarasi tumewahimiza kuhakikisha wanamalizia miradi hii na vijiji viweze kuwashwa ili tuweze kumaliza kabisa mradi huu. Kwa hiyo, tunafuatilia kwa karibu na tutaendelea kufuatilia kuhakikisha kwamba vijiji hivi sasa vinakamilika na vinawashwa umeme, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sophia.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama alivyouliza swali la msingi, Kijiji, Kata ya Kinyala ni kata ambayo ni kubwa sana na kiukweli *transformer* mpaka sasa haijafika. Mheshimiwa Naibu Waziri, ninajua weledi wako wa kazi, ni lini mtatuletea *transformer* hiyo ili watu hawa wa Kinyala waweze kupata umeme?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa swali zuri la Mheshimiwa Mbunge, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge baada ya hapa nitafuatilia kwa Meneja wa Wilaya na Meneja wa Mkoa, kuhakikisha kama kweli *transformer* haijafika basi mkandarasi aweze kuharakisha, aweze kupeleka na wananchi hawa waweze kupata umeme kwenye hivi vijiji ambavyo miradi inaendelea, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Wizara ya Maji, Mheshimiwa Josephat Kandege, kwa niaba yake Mheshimiwa Shally.

Na. 140

**Uhitaji wa Chanzo cha Uhakika cha Maji ya Ziwa Tanganyika**

**MHE. SHALLY J. RAYMOND K.n.y. MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE** aliuliza: -

Je, lini chanzo cha uhakika cha maji ya Ziwa Tanganyika kitatumika katika Vijiji vya Mwambao wa Ziwa na maeneo mengine Mkoa wa Rukwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, dhamira ya Serikali ni kutumia vyanzo vya maji vya uhakika katika utekelezaji wa miradi ya maji nchini ikiwemo mito na maziwa. Katika kutimiza azma hiyo, Serikali tayari imeanza na inaendelea kutumia vyanzo hivyo kwa ajili ya kusambaza maji, huduma ya maji safi na salama kwenye maeneo mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Mkoa wa Rukwa, chanzo cha Ziwa Tanganyika kimenufaisha wananchi wapatao 47,349 waishio kwenye mwambao wa ziwa hilo kupitia utekelezaji wa Miradi ya Maji ya Kipwa, Kapele Wilayani Kalambo, Kabwe, *Kabwe camp*, Udachi, Mkinga, Majengo, Ntanganyika, Kalungu, Mtakuja, Kamwanda, Kichangani na Itete Wilaya ya Nkasi. Vilevile Serikali ipo kwenye hatua za mwisho za kuajiri mtaalam mshauri kwa ajili ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina *(feasibility study and detailed design)* kwa ajili ya mradi mkubwa wa maji utakaotumia chanzo cha Ziwa Tanganyika kwa lengo la kuhudumia mikoa ya Rukwa na Katavi.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, katika mwaka wa fedha 2024/2025 Serikali itatekeleza miradi ya maji kwa kutumia chanzo cha Ziwa Tanganyika itakayonufaisha vijiji 16 vya Kazovu, Kisambala, Mandakerenge, Msamba, Uhuru, Utinta, Kalila, Isaba, Izinga, Kala, Kasanga, Muzi, Kisala, Samazi, Pamoja na Kipanga na Katili.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Shally.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na niishukuru Serikali kwa majibu ya uhakika yanayotia moyo na nina hakika kwamba wananchi wa kule Kalambo wameyasikia.

Kwa kuwa tatizo lililopo kule Kalambo mMoani Rukwa, linafanana kabisa na tatizo lililopo katika tambarare ya Mkoa wa Kilimanjaro Wilaya ya Rombo na Wilaya ile tuna Ziwa Chala, ni lini sasa Serikali hii itatumia Ziwa Chala kuwapatia maji safi na salama wananchi wa Wilaya ya Tambarare ya Rombo? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa kama ambavyo nimejibu katika jibu la msingi, Serikali ipo tayari kutumia vyanzo vya maji vya uhakika katika kuhakikisha kwamba tunawasogezea huduma ya maji wananchi katika maeneo mbalimbali wenye maeneo ya kijiografia yanayofanana na Kalambo kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge mama yangu alivyopendekeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Ziwa Chala tunapokea ushauri huo kama Serikali tutaenda kulifanyia kazi tuone urahisi zaidi kwa namna ambayo maji yataweza kuwafikia kwa gharama ambayo itakuwa inakubalika kwa wananchi wa eneo husika, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Anatropia.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Vijiji vingi vya Wilaya ya Kyerwa havina maji safi na salama licha ya kwamba tuna vyanzo vya kuaminika vya Mto Kagera lakini pia na Ziwa Victoria. Kata za Songambele, Lwabwele, Nyakatuntu, Businde, Bugara kuna changamoto kubwa ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kujua ni lini Serikali itatumia hivi vyanzo vya uhakika vya mto Kagera na Ziwa Victoria kuwapatia wananchi wa Wilaya ya Kyerwa maji safi na salama? Nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Mbunge kwa swali zuri kwa ajili ya wananchi wa Kyerwa lakini pia Serikali imeshatoa kibali cha kutangazwa kwa Mradi wa Songambele wa shilingi bilioni 1.9 lakini vilevile Mradi wa Kigologolo kisima kimeshachimbwa. Nawapongeza sana waheshimiwa wabunge wote kwa kushirikiana na Mbunge wa Jimbo, Mheshimiwa Bilakwate, mmefuatilia kwa ukaribu sana mradi huu na sisi kama Serikali tutaendelea kuhakikisha kwamba tunawaunga mkono... *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kifupi, kwa kifupi sana.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kassinge.

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi ya swali moja la nyongeza kwa Mheshimiwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kata ya Lihilimaliyao katika Jimbo la Kilwa Kusini ndiyo kata yenye changamoto ya ukosefu wa maji iliyokithiri zaidi. Hapa Bungeni uliahidi kwamba...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa uliza swali lako.

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nauliza swali, lini Mheshimiwa Naibu Waziri atatekeleza ahadi ya kwenda Lihilimaliyao, Kilwa Kusini ili tukatatue changamoto ya maji katika kata hiyo? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napokea wito wa Mheshimiwa Mbunge na baada ya Bunge lako Tukufu kuahirishwa tutapanga ratiba kwa ajili ya kufika katika eneo hilo na kujionea hali halisi.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea Mheshimiwa Anastazia Wambura.

Na. 141

**Mradi wa Maji Makonde**

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itakamilisha utekelezaji wa Mradi wa Maji Makonde?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea na utekelezaji wa Mradi wa Maji wa Makonde kupitia Mradi wa Maji wa Miji 28. Kazi zinazotekelezwa katika mradi huo ni pamoja na uchimbaji wa visima virefu vitatu vyenye uwezo wa kuzalisha maji lita milioni 26 kwa siku, ujenzi wa matanki manne yenye jumla ya ujazo wa lita milioni 13 na ulazaji wa mabomba umbali wa kilometa 81.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa mradi huo umefikia wastani wa 31% ambapo unatarajiwa kukamilika mwezi Disemba, 2025 na kunufaisha wananchi waishio kwenye Wilaya za Newala, Tandahimba pamoja na Mji wa Nyanyamba. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Wambura.

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika kufuatilia kwangu hali ya utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi, nimekuta kwamba Mradi huu wa Makonde ulikuwa ukamilike mwaka 2024, lakini mkandarasi ameongezewa muda na ni kutokana na hali ya ucheleweshaji wa malipo.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kwamba sasa mradi huu unatekelezwa na unakamilika Disemba, 2025 kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, ningependa nifahamu kwamba je, Serikali imeweka utaratibu gani kuhakikisha kwamba miradi mingine ikiwa ni pamoja na ule wa Mto Ruvuma yote inakamilika kwa wakati? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Anastazia, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Mbunge kwa kuendelea kufuatilia kwa ukaribu sana utekelezaji wa miradi hii kwa faida ya wananchi wa eneo lake. Ni kweli kabisa mradi huu unaenda kukamilika Disemba, 2025 na

Mheshimiwa Mbunge amegusia namna ambavyo ulitakiwa kukamilika mwaka 2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huu *nature* yake ni *design and build*. Maana yake kwamba tunakuwa tunafanya *design* na ndiyo tunaendelea kujenga, kwa hiyo, muda ambao ulikuwa umetolewa wa kwanza wa kufanya *feasibility study* na kuja kufanyia mapitio ulisababisha tufanye *extension* ambapo mradi huu tunauhakika utaenda kukamilika mwaka 2025...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, utumie muda mfupi sana kueleza, *it a very simple question*, mwambie tu *design* inakwisha muda fulani basi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

Kwa upande wa swali la pili ni kwamba miradi yote nchini tumeweka mkakati wa kuhakikisha kwamba fedha zinapelekwa katika miradi mbalimbali ili iweze kukamilika kwa wakati, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Bilakwate.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Wilaya ya Kyerwa tunamradi wa vijiji 37 wenye thamani ya shilingi bilioni 58. Mradi huu unaenda kuhudumia Kata ya Kyerwa, Yaluzumbula, Nyakatuntu mpaka Kamuli. Mradi huu ni lini utatangazwa ili wananchi waweze kupata maji safi na salama?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ni mradi muhimu sana tunatambua na Wizara imeshaandika kuomba kibali ili uweze kutangazwa kwa ajili ya kuhakikisha kwamba unaanza kujengwa kwa ajili ya maslahi ya wananchi wa Kyerwa, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Maimuna.

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, kwa sababu Mradi wa Maji wa Makonde ni mradi ambao ni wa muda mrefu, Serikali mwaka 2022 ilituchimbia visima kwenye Kijiji cha Mpalu na Lochinu kwenye Jimbo la Newala Vijijini, lakini visima vile havijasambaza maji mpaka kwa wananchi. Je, ni lini Serikali itapeleka miundombinu ili yale maji kwenye visima yafike kwa wananchi? Nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, visima vyote ambavyo tumeshavichimba na tumesha-*test*, tumeshafanya *pump test*, tunaenda kuhakikisha kwamba sasa tunaenda kujenga *a point source* kwa ajili ya wananchi kupata huduma ya maji safi na salama, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Dorothy Kilave.

Na. 142

**Kuweka Mita za Maji Kama za LUKU**

**MHE. DOROTHY G. KILAVE** aliuliza: -

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuweka mita za maji kama za LUKU ili kuwawezesha wananchi kulipa bili za maji kulingana na matumizi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeendelea na ufungaji wa dira za malipo ya kabla *(pre paid water meters)* ambapo hadi kufikia mwezi Juni, 2024 jumla ya dira 14,914 zilikuwa zimefungwa kwa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira nchini pamoja na *RUWASA* ambapo kati ya hizo, dira 11,861 zilifungwa kwa Mamlaka ya Maji Safi na Miji Mikuu ya Mikoa, dira 325 zilifungwa na Mamlaka za Miradi ya Kitaifa, dira 692 zilifungwa na Mamlaka ya Maji ya Miji Mikuu ya Wilaya na dira 50 Mamlaka za Miji Midogo. Vilevile kwa upande wa vijjijni jumla ya dira 1,986 zilifungwa kwa Vyombo vya Watoa Huduma ya Maji Ngazi ya Jamii *(CBWSO)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa Serikali imekamilisha uandaaji wa andiko dhana *(concept note)* pamoja na mpango mkakati sambamba na kutengeneza mfumo wa ankara wa kuendesha dira za malipo ya kabla ifikapo Julai, 2025. Aidha, Serikali inaendelea kusimamia, kusisitiza na kuziwezesha Mamlaka za Maji na Usafi wa Mazingira pamoja na Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini *(RUWASA)* kuhakikisha zinaongeza kasi ya ufungaji wa dira za malipo ya kabla ili kuwawezesha wananchi kulipa ankara za maji kulingana na matumizi na kuboresha usimamizi wa mauzo na makusanyo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kilave.

**MHE. DOROTHY G. KILAVE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa majibu mazuri, lakini je, kutokana na wananchi wa Jimbo la Temeke, kuna malalamiko ya kwamba wananlipa maji ambavyo hawatumii kihalali.

Je, ni lini sasa ndani ya Jimbo letu la Temeke mtaanza kufunga hizi *pre paid meters*?

Swali langu la pili, ni lini sasa mtafunga nyumba hizi ambazo zinamilikiwa na taasisi za Serikali, mfano *TBA*, wapangaji wanapoanza kupanga nyumba wanakuta kuna bili zile za nyuma, je, ni lini sasa mtafunga hizi *meter* katika hizi nyumba za Serikali ili anayepanga asikute ile bili inayotokana na aliyepanga. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatambua changamoto ya bili kwa wananchi lakini vile vile kwa kufuatia maelekezo ya Dkt. Samia Suluhu Hassan, ya kupunguza malalamiko kwa kufunga *pre paid water meters* ili kusaidia wananchi wasiwe wanawekewa bili ambazo haziendani na matumizi yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali tayari kupitia Wizara imeshaandika andiko dhana kama ambavyo nimejibu katika jibu la msingi na tayari kuna maeneo ambayo tayari tumeshaanza kufunga kama ambavyo nimetaja, lakini kwenye taasisi na siyo *TBA* peke yake, taasisi nyingi ambazo tunaamini kwamba namna ya kudaiana inakuwa na changamoto, sisi huko ndiyo kipaumbele chetu ili kuhakikisha kwamba hata yale mapato ambayo yanatokana na malipo yao yatatusaidia katika uendeshaji wa miradi yetu ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Temeke nikuhakikishie kwamba mfumo huu utakapokamilika hatutaki tuwe na mifumo mingi ndani ya nchi moja, ndani ya mamlaka mbalimbali, tunataka tuwe na mfumo mmoja ambapo kama Moshi, Mwanza, Dar es Salaam wote watatumia mfumo mmoja ili kuhakikisha kwamba tuna uwezo wa ku-*regulate pre paid water meter* zote ambazo tunaweza kuzifunga kwa wananchi na kuweza ku-*monitor* utumiaji na upatikanaji wa mapato kulingana na matumizi ya wananchi husika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Jackson Kiswaga.

Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Jackson Kiswaga. Mheshimiwa Justin.

Na. 143

**Ujenzi wa Bwawa la Umwagiliaji Kijiji cha Magubike - Kalenga**

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA K.n.y. MHE. JACKSON G. KISWAGA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa bwawa la umwagiliaji katika Kijiji cha Magubike Kata ya Nzihi – Kalenga?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KILIMO** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jackson Kiswaga, Mbunge wa Kalenga, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Kilimo kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imetenga fedha kwa ajili ya kukamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa Bwawa la Magubike pamoja na skimu kwa lengo la kuanza ujenzi katika mwaka wa fedha 2024/2025. Baada ya ujenzi huo kukamilika wananchi 1,200 watanufaika na kilimo cha umwagiliaji.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Justin.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu mradi huu Mradi wa Magubike umechukua muda mrefu kidogo, je, Serikali haioni umuhimu wa kuharakisha ujenzi wa mradi huu ili wananchi wapate huduma?

Swali la pili, Mradi wa Umwagiliaji wa Mgambalenga ambao ujenzi wake umekuwa ukisuasua, je, Serikali inampango gani

wakumwambia mkandarasi yule kuharakisha ujenzi kwa sababu tayari ana mkataba na analipwa. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba mradi huu umekuwa wa muda mrefu lakini nataka niwahakikishie kwamba mwaka huu unatangazwa na mwaka huu utaanza kutekelezwa, lakini kuhusu Mgambalenga kulikuwa kuna matatizo ya kifedha nashukuru Wizara ya Fedha wameshatuandalia utaratibu wa kutupatia fedha, mkandarasi atarudi kuwa *effective* kufanya kazi yake. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. *Engineer* Samweli.

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Je, Mheshimiwa Waziri, umeniahidi mara kadhaa kuhusu Mradi wa Bwawa la Ngindababiek, lini tutapata fedha ili mradi huo uweze kujengwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Mbunge wa Hanang kama ifuatavyo; jana mimi na yeye tulikuwa pamoja, kaacha barua ofisini na nimeshatoa maelekezo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Profesa.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru, je, Serikali ina mkakati gani wa kuanza ujenzi wa Skimu

ya Makeresho ambayo itakuwa msaada mkubwa sana kwa wakulima wa Kahawa katika Kata ya Kibosho Magharibi? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumjibu Profesa Ndakidemi, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Makeresho tumeshaitangaza na sasa hivi ipo kwenye mfumo, tunasubiri mkandarasi apatikane *In ShaaAllah* mwaka huu wa fedha atakuwa *site*.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Van Zeeland.

**MHE. JONAS V. ZEELAND:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, naomba kuuliza swali dogo la nyongeza.

Katika Kata ya Mkindo tuna mradi wa umwagiliaji wenye thamani ya shilingi bilioni 5.6, mkandarasi toka amepewa kazi mwaka juzi mpaka sasa hivi hajafika hata 50%. Je, lini atakamilisha ili mradi huu uweze kuwasaidia wakulima wetu wa Mkindo? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimjibu Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli mkandarasi amekuwa akisuasua na amekuwa akitafuta sababu za kuhalalisha kuchelewesha utekelezaji wa mradi. Nataka tu nimhakikishie kuwa Wizara tumekuwa *very close* na yeye na si muda mrefu tuta-*unlock* matatizo yaliyopo kati ya sisi na yeye na ikishindikana tutatafuta njia sahihi ya kuachana ili hiyo ndoa ife, tutafute mkandarasi mwingine.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Daimu Mpakate.

Na. 144

**Ujenzi wa Ghala la Mazao – Tunduru**

**MHE. DAIMU I. MPAKATE** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kukamilisha ujenzi wa ghala la mazao Wilayani Tunduru lililoanza kujengwa na Bodi ya Korosho mwaka 2014?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate, Mbunge wa Tunduru Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa ghala la Tunduru ulisimama baada ya Serikali kusitisha Mfuko wa Kuendeleza zao la Korosho ambao moja ya majukumu yake ilikuwa ni ujenzi wa ghala. Aidha, Serikali imekakilisha majadiliano na mkandarasi aliyekuwa anajenga ghala hilo ili kuruhusu ujenzi kuendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha wa 2024/2025, Serikali imetenga jumla ya shilingi 5,000,000,000 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa ghala za korosho katika Halmashauri ya Mkuranga, Mkinga na Tunduru ambazo ujenzi wake ulianza mwaka 2015. Bodi ya Korosho inakamilisha taratibu za manunuzi ili kuanza ujenzi wa ghala hizo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mpakate.

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na nashukuru kwa majibu mazuri, lakini nilikuwa namwomba Waziri alete muda *specific* ni lini mchakato huu utakamilika?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa mfumo wa stakabadhi ghalani ni muhimu sana kuwa na maghala ya kisasa

hasa kwenye maeneo ya vijiji. Ni nini mkakati wa Serikali kujenga maghala katika vijiji mbalimbali vilivyopo katika Jimbo la Tunduru Kusini? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mpakate, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lini utakamilika.

Mheshimiwa Naini Spika, siwezi kusema lini utakamilika wakati hata kurudi *site* hatujarudi. Tumerudisha mfuko pamoja na ninalishukuru Bunge lako Tukufu Mfuko wa Kuendeleza Zao la Korosho ulikuwa umefutwa sasa tunaanza kupata fedha na nimesema katika bajeti ya mwaka huu 2024/2025 tumetenga fedha kwa ajili kuanza kujenga maghala haya yote matatu ambayo yalikuwa yamesimama toka mwaka 2015.

Kwa hiyo, ni matarijio ya Serikali kwamba ndani ya mwaka huu wa fedha wakandarasi watarudi *site* kwa ajili ya kuanza utekelezaji wa mradi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu maghala ya vijijini, nataka nimuombe tu Mheshimiwa Mbunge hata kwenye kikao cha wadau wa korosho tulijadili, Serikali inaendelea kujenga maghala vijijini kila mwaka lakini jambo la misingi ambalo tunalifanya sasa hivi, kwanza ni kufanya *audit* ya maghala yaliyojengwa na Serikali ambayo yamebaki vijijini yamekuwa *idle* ili kuweza kuyatumia na kuyarasimisha rasmi na kufanyia *rehabilitation.* Mkoa wake tu katika mwaka wa fedha uliopita tumejenga maghala zaidi ya 28 ingawa Jimbo lake halikupata katika hayo maghala.

Kwa hiyo, nimhakikishie ni mpango wa Serikali kuendelea kujenga maghala vijijini ili kuondoa tatizo la stakabadhi ya ghala, lakini vilevile matatizo ya uhifadhi wa mazao ya wakulima.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Chikota.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na naipongeza Serikali kwa kuanza utekelezaji mradi wa kongani ya viwanda vya korosho pale Malanje na kuna ujenzi wa maghala mawili umeshaanza, lakini kwa ramani ya pale tumeona kwamba kutakuwa na ujenzi wa maghala 10.

Je, Wizara ina mpango gani wa kupeleka fedha nyingine za ujenzi wa maghala nane yaliyobaki? Nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimuombe Mheshimiwa Chikota, Mbunge wa Nanyamba jambo moja; kwanza, tukamilishe mradi ambao tumeuanza, halafu tutafanya miradi mingine baada ya kukamilisha mradi ambao tumeanza hivi sasa. Ni mpango wa Serikali kuhakikisha kwamba *Malanje Industrial Park* inakamilika na *private sector* wameanza kuja tutawahusisha na wenyewe katika ujenzi wa maghala.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Mheshimiwa *Engineer* Mwanaisha Ulenge.

Na. 145

**Tafiti Zinazofanywa na Wanafunzi Mbalimbali Nchini**

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE** aliuliza:-

Je, lini Serikali itachakata tafiti zinazofanywa na wanafunzi ili kuchochea ugunduzi na ukuaji wa teknolojia katika sekta mbalimbali nchini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kufanya utafiti na kutumia matokeo ya utafiti ili kuongeza

maendeleo ya sayansi na teknolojia nchini, pamoja na juhudi nyingine, Serikali imeendelea kuboresha miundombinu, kuweka vifaa na vifaa stahiki pamoja na kuandaa wataalamu wa utafiti kwa kuwawezesha kupata mafunzo ya muda mfupi na mrefu ili tafiti zinazofanyika vyuoni zikiwemo tafiti za wanafunzi ziwe na mchango katika maendeleo ya teknolojia na ubunifu nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2023/2024 Serikali imewezesha kuanzishwa kwa vituo atamizi vipya 17 kwa ajili ya kukuza na kuendeleza ubunifu unaozalishwa nchini. Vituo atamizi vilivyopo katika Taasisi za Elimu na Mafunzo vinasaidia kuendeleza ubunifu na matokeo ya utafiti yanayotokana na kazi zinazofanywa na wanafunzi katika taasisi hizo. Hivyo, wanafunzi wanapata fursa ya kutumia elimu wanayoipata kwa maendeleo yao binafsi na Taifa kwa ujumla. Mafanikio yaliyotokana na kuanzishwa kwa vituo hivyo ni pamoja na kuanzishwa kwa makampuni mapya 94 yanayotokana na ubunifu na hivyo kutoa ajira za moja kwa moja kwa vijana takribani 600. Nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa *Engineer* Mwanaisha.

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imesema inaweka vifaa kwenye vyuo vyetu, lakini je, haioni haja sasa ya kuhakikisha vyuo vyote nchini vinakuwa na *database* ya tafiti mbalimbali zilizofanywa na wanafunzi kwa ajili ya matumizi ya baadaye? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili, ili kutengeneza mnyororo wa thamani wa matumizi bora ya tafiti na kuuchochea ubunifu na ugunduzi nchini.

Je, Serikali haioni haja sasa ya ku-*pioneer* kusimamia uanzishaji wa jamii za wanataaluma wa sekta mbalimbali na kuwaunganisha na wanafunzi wa vyuo ili kuchochea ubunifu na ugunduzi nchini? Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Wazirin kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nikijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa *Engineer* Mwanaisha Ulenge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nimuondoe hofu Mheshimiwa Mbunge kuhusiana na suala la kuanziasha kanzidata, tayari Serikali imeshafanya kazi hii. Hivi sasa tunavyozungumza vyuo vingi sana vya elimu ya juu pamoja na taasisi zetu za elimu ya juu tayari zimeanza kuwa na hizi *database* au kanzidata ambazo zitakuwa zinahifadhi hizi *soft copy* au nakala laini za utafiti na ubunifu. Hivi sasa tumeanza kwa ngazi ile ya Shahada zile za Umahiri *(Masters)* pamoja na zile za Uzamivu *(Ph.D)* na tumeziagiza taasisi zetu zote ziweze kuanzisha kanzidata hizi ili kuhakikisha kwamba zile tafiti na bunifu ninaweza kutunzwa siyo hizi tu za sasa hata zile za miaka ya nyuma tumeanza ku-*digitalize* ili kuweza kuzitunza katika kanzidata hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo la pili ambalo anataka kufahamu kama Serikali ina mpango gani juu ya uendelezaji, lakini kutengeneza *linkage* baina ya wanataaluma na wale ambao wanafanya kazi kule viwandani. Nimuondoe hofu Mheshimiwa Mbunge pamoja na Bunge lako Tukufu, Serikali tayari imetoa mwongozo kwanza wa uanzishwaji wa vikundi hivi au kampuni hivi tunaziita kampuni tanzu katika Taasisi zetu za Elimu ya Juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia mradi wetu wa mageuzi makubwa ya kiuchumi *(HEET)* pamoja na ule wa *EASTRIP* tumenzisha makampuni tanzu kwenye taasisi zetu za elimu ya juu kwa lengo la kutengeneza wigo wa wanataaluma wetu na watafiti kuwa na *linkage* na viwanda na maeneo mengine ya sekta binafsi ili kuhakikisha zile tafiti na bunifu zao zinapelekwa kule, lakini zinaweza kutumika katika maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tayari ukienda kwenye Taasisi yetu ya *DIT,* Nelson Mandela pale Arusha, lakini *University of Dar es*

*Salaam* hata ukienda *MUST* kule Mbeya wana Makampuni haya ambayo yanatengeneza *linkage* baina ya taasisi zetu za kitaaluma na viwanda vyetu. Nakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa kabla sijamwita Waziri wa Fedha, naomba kuwatambua wageni kutokana na wageni kuwa wengi hawa watoke waingie wengine.

Wageni waliokaa Jukwaa la Spika, ni mgeni wa Mheshimiwa Gulam Abbas Tarimba, Naibu Meya kutoka Kinondoni Jijini Dar es Saalam. *(Makofi)*

Wageni 10 wa Waheshimiwa Wabunge wa Temeke ambao mo Viongozi wa Kamati ya Siasa ya Wilaya; Ndugu Zena Yusufu Mgaya - Mwenyekiti wa CCM Wilaya; Ndugu George Sayi - Katibu wa CCM Wilaya; Ndugu Lawama Mikidadi - Mwenyekiti UWT; Ndugu Hamis Hamis - Mwenyekiti Wazazi; Ndugu Samweli Kiogolo - Mwenyekiti Vijana; Ndugu Jane Benjamin - Katibu UWT; Ndugu Emmanuel Itatiro - Katibu Wazazi; Ndugu Sayi Samba - Katibu Vijana; Ndugu Mussa Mtulya - Mjumbe Kamati ya Siasa na Ndugu Happy Nyema - Mjumbe Kamati ya Siasa, karibuni. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa George Ranwell Mwenisongole aambao ni walezi wake wakati anasoma nchini Marekani, hawa ni Ndugu Don Irwim Frontone, Ndugu Cynthia Lou Frontone na Ndugu Morris Swai – mkalimani, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge; wapo wageni 37 wa Mheshimiwa Omari Juma Kipanga - Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, hawa ni wapiga kura wake kutoka Jimbo la Mafia, Mkoa wa Pwani. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Ridhiwani Jakaya Kikwete, marafiki zake kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Askofu Mathias Gwajima, rafiki zake kutoka nchini Ghana, karibuni. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Noah Saputu Mollel, wapiga kura wake kutoka Arumeru Magharibi, Mkoani Arusha. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Dkt. Angeline Sylvester Lubala Mabula, watoto wake kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Wageni wengine wawili wa Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula, wapiga kura wake kutoka Ilemela, Jijini Mwanza, karibuni. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Abeid Ramadhani Ighondo, Mwenyekiti na Katibu wa Vijana Kata ya Mrama, Mkoa wa Singida. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Flatei Massay, wapiga kura wake kutoka Mbulu Vijijini. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Festo Sanga, marafiki zake kutoka Jijini Arusha. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Mohamed Suleiman Omar, Viongozi wa CCM kutoka Jimbo la Malindi, Mjini Zanzibar. *(Makofi)*

Wageni wanne wa Mhe. Juma Usonge Hamad, marafiki zake kutoka Gairo, Mkoa wa Morogoro. *(Makofi)*

Wageni watano wa Mheshimiwa Amandus Julius Chinguile, wapiga kura wake kutoka Nachingwea, Mkoa wa Lindi. *(Makofi)*

Wageni 14 wa Mheshimiwa Abdallah Jafari Chaurembo, familia yake kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Wageni 29 wa Mheshimiwa Justin Nyamoga, Wainjilisti wa Kanisa la KKKT, Dayosisi ya Iringa kutoka Ilolo, karibuni. *(Makofi)*

Wageni 37 wa Mheshimiwa Seif Khamis Said Gulamali na hawa ni Wakuu wa Idara na Vitengo kutoka Wilaya ya Igunga, Mkoa wa Tabora. *(Makofi)*

Wageni wengine 37 wa Mheshimiwa Dkt. Kabati, hawa ni Wanakwaya wa *Kagongwa SDA* kutoka Kahama, Mkoa wa Shinyanga, kutoka Kagongwa. *(Makofi)*

Wageni 126 wa Mheshimiwa Margaret Simwanza, Chama cha Wanawake Wamiliki wa Shule na Vyuo vya Kati *(TAWSCO)* kutoka Mikoa mbalimbali nchini. *(Makofi)*

Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; Ndugu Savia Onesmo kutoka Makulu Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Shirika la *Community Concern for Orphans and Development Association* kutoka Mkoa wa Njombe. *(Makofi)*

Wanafunzi 20 wa Chuo cha Maji kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea Wizara ya Fedha, Mheshimiwa Kuchauka.

Na. 146

**Uuzwaji wa Magari Mabovu**

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA** aliuliza:

Je, Serikali ina mpango gani wa kuyauza magari mabovu yaliyopo kwenye halmashauri zetu nchini na kwenye Ofisi za Serikali?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zuberi Mohamedi Kuchauka, Mbunge wa Liwale, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa miongozo iliyopo ya ufutaji na uondoshaji wa mali chakavu ikijumuisha vyombo vya moto katika halmashauri na taasisi za Serikali, Wizara ya Fedha ina jukumu la kuhakiki na kutoa vibali vya ufutaji na uondoshaji wa mali chakavu. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Wizara ya Fedha ilitoa jumla ya vibali vya kuondosha mali chakavu 160 katika Halmashauri na Ofisi za Serikali. Kati ya vibali hivyo, kulikuwa na vibali vya magari chakavu 976 yenye thamani ya shilingi bilioni 2.4. Aidha, magari chakavu 223 yenye thamani ya shilingi bilioni 1.6 yaliondoshwa kwa njia ya mnada kwa taasisi 54. Vilevile ufualitiaji na tathmini ya magari ya miradi ulifanyika na kubaini magari 339 yenye thamani ya shilingi 479,565,000 kuwa ni chakavu na taratibu za uondoshaji wake zinaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya Julai na Agosti, 2024 vibali 70 vya uondoshaji wa magari chakavu vimetolewa kwa halmashauri na Ofisi za Serikali. Aidha, Septemba, 2024 Wizara ya Fedha itaratibu na kusimamia minada kwenye taasisi 54 ya uondoshaji wa vyombo vya moto 150 katika mikoa tisa ambayo ni Dar es salaam, Mbeya, Arusha, Morogoro, Mtwara, Njombe, Lindi, Pwani na Dodoma, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kuchauka.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa majibu mazuri ya Serikali yanayoonesha kwamba kuna juhudi kubwa inafanyika, lakini kwa sababu ya magari haya ya mitambo hii kwenye halmashauri zetu huwa zinachukua muda mrefu sana kiasi kwamba inafanya kwamba Serikali ipate hasara na vingenevyo ni kuwa uchafu kwenye halmashauri zetu.

Je, ni mkakati upi unaofanywa na Serikali kuhakikisha magari haya yanaondolewa kwa wakati na Serikali isiendelee kupata hasara? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, mchakato mzima wa kuyaondoa hayo magari tangu gari linapooneka kwamba haliwezi kutengenezeka mpaka unaenda kuliingiza kwenye mnada mchakato huo unachukua muda gani? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Kuchauka, naomba nimpongeze kwa ufuatiliaji wa suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la kwanza ni wajibu wa taasisi husika na halmashauri wanaotakiwa kuzipitia na kubaini gari chakavu au vyombo vya moto chakavu na kuripoti kwa kufuata taratibu Serikalini. Kwa hiyo, nielekeze ama niwaombe ndugu zangu wanaoongoza taasisi hizo kufuatilia na kuhakiki, wakibaini kwamba gari hizo ni chakavu basi walete taarifa kwa Wizara ya Fedha, Wizara ya Fedha itahakiki na kutoa vibali kwa ajili ya kuuza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili, hakuna muda maalumu, sipokuwa vipo vigezo ambavyo vinaashiria kwamba sasa gari limekuwa chakavu vigezo hivyo kwa mfano kama *mileage* yaani kama imetembea kilometa zaidi ya 500,000, ama gari umri ambao imeishi umri mrefu zaidi ya miaka nane, lakini ajali kubwa, mazingira ya gari, lakini mabadiliko ya teknolojia, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kawawa.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, kwa kuwa magari haya yapo mengi pia katika Wizara na Taasisi za Serikali na tuna Vyuo vya *VETA* tulivyojenga nchini vinahitaji magari ya kufundishia.

Je, Serikali haioni ipo haja sasa ya baadhi ya magari haya yakapelekwa kwenye Vyuo vya *VETA* kwa ajili ya kufundishia utengenezaji wa *panel beating* (uundaji wa magari) na *mechanics* na umeme wa magari? Wakati ndio huu. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Kawawa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Kawawa ametoa ushauri, ushauri wake umepokelewa tunaenda kuufanyia kazi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mheshimiwa Stella Fiyao.

Na. 147

**Hitaji la Uwanja wa Michezo – Ileje**

**MHE. STELLA S. FIYAO** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga Uwanja wa Michezo Wilayani Ileje?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, jukumu la ujenzi wa miundombinu ya michezo ni la Serikali ikiwemo Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kushirikiana na wadau wa sekta ya michezo, taasisi, mashirika na watu binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa Serikali ipo katika ukarabati wa viwanja vya Benjamin Mkapa pamoja na Uhuru Jijini Dar es Salaam, ujenzi wa uwanja wa Arusha na ukarabati viwanja vingine vitano vya mazoezi kwa ajili ya mashindano ya *CHAN 2025* na *AFCON 2027*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo basi, Serikali inaishauri Halmashauri na Wilaya ya Ileje kutenga fungu katika bajeti yake ili kutekeleza mradi ya ujenzi wa kiwanja cha michezo wakishirikiana na wadau wa maendeleo. Wizara ipo tayari kuwapatia wataalamu wa miundombinu ya michezo kuwashauri ipasavyo

na itakapofika hatua ya utekelezaji mradi wa ujenzi wa uwanja huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia Bunge lako Tukufu nazipongeza Halmashauri za Wilaya za Kinondoni kwa kujenga Uwanja wa *KMC,* Bukoba Mjini kwa kujenga Uwanja wa Kaitaba, Nyamagana kwa kujenga Uwanja wa Nyamagana, Halmashauri ya Mji-Babati kwa kuwanja Uwanja wa *Tanzanite* na Halmashauri ya Namungo kujenga Uwanja wa *Majaliwa Stadium)* kwa kuonyesha mfano bora na sasa wanamiliki na kuendesha viwanja vya michezo vya kisasa. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Stella.

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza halmashauri nyingi hazina uwezo wa kujijengea viwanja zenyewe ikiwemo Halmashauri ya Wilaya ya Ileje, sasa nataka kujua mpango wa Serikali ni upi kuhakikisha mnazishawishi taasisi binafsi ili zije ziwekeze uwanja katika Halmashauri ya Wilaya ya Ileje hasa ukizingatia kwamba Ileje ni Wilaya ambayo ipo mpakani baina ya Malawi na Tanzania. Je, hamuoni jambo hili linaweza kuwa ni fursa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Stella tunajua Ileje ipo wapi, uliza swali.

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Naibu Spika, tayari nimeshauliza swali la kwanza.

Swali langu la pili, Halmashauri ya Mji wa Tunduma imetenga viwanja kwa ajili ya michezo kikiwepo kiwanja cha Kata ya Chapa katika Halmashauri ya Mji wa Tunduma. Nataka kujua, Serikali hamuoni umuhimu wa kuharakisha zoezi hili ili uwanja uweze kujengwa na wananchi waweze kunufaika kama ilivyopagwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru Mheshimiwa Stella kwa maswali yake mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali, Wizara yenye dhamana ya utamaduni, Sanaa na michezo kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, TAMISEMI tupo katika mkakati wa kuhakikisha kwamba tunakuwa na *sports centre* moja katika kila halmashauri ikijumuisha viwanja au michezo yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, makakati huu utakapokamilika tutaweza kuuleta katika bajeti ya mwakani na unaweza ukaanza kutekelezwa kwa Serikali kushirikiana na taasisi binafsi na wadau wa maendeleo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tarimba.

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa nafsai ya kuweza kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri ametaja juhudi iliyofanywa na Halmashauri ya Manispaa pale Kinondoni ambapo jumla ya shilingi bilioni 10.1 zitatumika uwanja ule ukiwa umekamilika. Ni uwanja wa mfano mpaka *Simba Sports Club* inakwenda kucheza pale.

Sasa Mheshimiwa Waziri, ningekuomba uipongeze Halmashauri ya Manispaa kisawa sawa, halmashauri inayoongozwa na Mstahiki Meya Songoro Mnyonge, Naibu Meya Michael Urio pamoja na Mkurugenzi Hanifa Hamza na Mbunge wao Tarimba Abbas…

**NAIBU SPIKA:** Uliza swali Mheshimiwa Tarimba.

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nirudie tena. Nichukue nafasi hii kuipongeza Halmashauri ya Kinondoni inayoongozwa na Mheshimiwa Mbunge Abbas Gulam Tarimba kwa kujenga uwanja mzuri wa kisasa ambao umetumika kwenye mashindano ya *CECAFA* na sasa hivi unatumika na vilabu vyetu vikubwa vya Simba na Yanga. Halmashauri nyingine tuige mfano Halmashauri ya Kinondoni. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Lakini kwa kweli Kinondoni imefanya vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, ni kwa nini Serikali isiweke kipaumbele cha ujenzi wa uwanja wa kisasa Wilayani Butiama ambapo ni kwa Baba wa Taifa katika kumuenzi ili kiweze kutumika kwenye mashindano ya *AFCON* na kuweza kutoa fursa kwa watu wengi kutembelea hata kaburi la Baba wa Taifa na kukuza utalii? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nirejee tena, jukumu la msingi na la awali ni la halmashauri husika na ndiyo maana nimezipongeza halmashauri ambazo zimefanya vizuri ikiwemo Halmashauri ya Ruangwa ambayo inaongozwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu Kassim Majaliwa Majaliwa, kwa kujenga uwanja mzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kama Wizara na Serikali tutashirikiana na halmashauri ya Butiama kuwapa ushauri na kuwatafutia wadau ili wafanye kama halmashauri hizi nyingine ya Ruangwa, Kinondoni, Nyamagana, Babati na halmashauri nyingine. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Na Bunju?

Waheshimiwa tunaendelea, Wizara ya Mifugo, Mheshimiwa Zakaria Kamonga.

Na. 148

**Ujenzi wa Mahema na Vichanja vya Kukaushia Samaki – Ludewa**

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itajenga vichanja na mahema ya kisasa ya kukaushia samaki na dagaa kwa kutumia nishati ya umeme na jua Ludewa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kuboresha na kujenga miundombinu ya uvuvi katika maeneo mbalimbali nchini ikiwemo mwambao wa Ziwa Nyasa. Miundombinu ya mahema na vichanja vya kukaushia samaki na dagaa husaidia kupunguza upotevu wa mazao ya uvuvi, kuongeza ubora, thamani na kuboresha biashara yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2024/2025 Serikali haina mpango wa kujenga vichanja na mahema ya kukaushia dagaa katika Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa. Aidha, Serikali inatekeleza mpango wa kupunguza upotevu wa mazao ya uvuvi na kuboresha biashara ya mazao hayo katika halmashauri hiyo ambapo imeanza ujenzi wa Soko la Samaki Manda katika Kijiji cha Nsungu, Kata ya Manda kuanzia mwaka wa fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia umuhimu wa miundombinu hii, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa Wizara yangu itaendelea na jitihada za kuboresha miundombinu ya uvuvi kulingana na upatikanaji wa fedha. Aidha, ninaomba Halmashauri ya Ludewa itambue umuhimu ya miundombinu ya mahema na vichanja vya kukaushia samaki na

dagaa na kuiweka kwenye miradi yake ya kimkakati kwa kutenga fedha kupitia mapato ya ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kamonga.

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi na nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kutoa shilingi milioni 800 kwa ajili ya ujenzi wa soko la samaki pale Manda. Pamoja na hilo nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa sasa Serikali imejenga soko hili la kisasa, je, ni lini Wizara itatuma wataalamu kwenda kutoa elimu ya ufugaji wa samaki kwa vizimba kwa wananchi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, ni lini Serikali itakwenda kutoa elimu ya uhifadhi wa mazalia ya samaki kwa wananchi ili kuweza kuongeza idadi ya samaki kwenye Ziwa Nyasa? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, tumepokea ombi la Mheshimiwa Mbunge na baada ya Bunge hili kuhitimishwa tutatuma wataalamu kwenda kutoa elimu ya vizimba ili wananchi wa eneo hilo waweze kupata elimu ya vizimba, lakini kwa taarifa tu ni kwamba baada ya mwezi wa tisa tayari utafiti wa namna gani vizimba vitakaa katika maeneo gani ya Ziwa Nyasa vitakuwa vimekamilika na wananchi wanaozunguka maeneo hayo wataruhusiwa sasa kuchukuwa vizimba kwa ajili ya kwenda kuweka katika Ziwa Nyasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili la pili la kutoa elimu, Wizara imeendelea kutoa elimu kwa wavuvi katika maeneo mbalimbali nchini na hususani katika eneo la Mheshimiwa Mbunge kule Ludewa tutatuma wataalamu wataenda kutoa elimu na baada ya Bunge hili Tukufu tuwasiliane Mheshimiwa Mbunge tuone

wavuvi gani wanahitaji elimu ili waweze kupatiwa elimu katika maeneo hayo, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Zodo.

**MHE. MWANTUMU M. ZODO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, je, ni lini Serikali itakwenda kujenga vichanja vya kuanikia samaki na dagaa kwa ukanda wetu wa Pwani hasa Pwani ya Tanga kwa maeneo ya Mkinga, Muheza, Tanga pamoja na Pangani kama ilivyotuahidi? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema katika jibu la msingi kwamba kwa sasa Serikali haina mpango wa kujenga vichanja isipokuwa tunahamasisha halmashauri husika zijikite kwenye kuweka kwenye miradi wa mkakati kujenga vichanja hivyo kwa sababu ndiyo vinasidia watu hao, lakini pia halmashauri zinajipatia mapato kupitia vichanja hivyo, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Assa Makanika.

Na. 149

**Fidia kwa Wananchi Walioguswa na Ujenzi wa Barabara ya Kigoma – Kasulu**

**MHE. KAVEJURU E. FELIX K.n.y. MHE. ASSA N. MAKANIKA** aliuliza: -

Je, nini mpango wa fidia kwa wananchi walioguswa na ujenzi wa Barabara ya Kigoma -Kasulu ambao nyumba zao zimewekewa X?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** aljibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Barabara Na. 13 ya mwaka 2007 na kanuni zake za mwaka 2009 iliongeza upana wa eneo la hifadhi ya barabara kuu na za mkoa kutoka meta 45 hadi 60 ikiwa na nyongeza ya meta 7.5 kutoka katikati ya barabara kila upande. Kufuatia utekelezaji wa sheria hii, alama ya "X" yenye rangi ya kijani iliwekwa kwenye nyumba zote za wananchi zilizopo katika eneo hii ikiwa na maana kuwa wananchi hao waendelee kuwepo katika eneo hilo hadi watakapolipwa fidia, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Felix.

**MHE. KAVEJURU E. FELIX:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwezi Julai, 2024 Makamu wa Rais Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango akiwa ziarani Mkoani Kigoma akiwa kwenye *centre* ya Mnanila katika Jimbo la Buhigwe aliagiza Wizara ya Ujenzi ilipe fidia wananchi 120 ambao walivunjiwa vibanda vyao kwenye mradi wa ujenzi wa barabara ya Kigoma – Manyovu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lini Serikali itawalipa wananchi hawa? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli maelekezo hayo alitoa Makamau wa Rais, lakini cha kwanza ambacho kimetufanya alielekeza kwanza tukutane na hao wanaodai ili tuweze kujua hasa wanataka nini.

Mheshimiwa Naibu Spika, tayari tumeshakutana nao, tumeshaongea nao, kwa hiyo, tutakapokuwa tumekamilisha na kujiridhisha kwamba kila mtu anataka nini basi wale wanaostahili kupata fidia watapata fidia yao. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Seif Gulamali.

Na. 150

**Ujenzi wa Barabara ya Choma – Ziba na Ziba Puge**

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI** aliuliza: -

Je, lini ujenzi wa barabara ya lami kutoka Choma - Ziba na Ziba - Puge utaanza?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa Barabara ya Puge – Ziba – Choma yenye urefu wa kilometa 109 unatekelezwa kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha. Katika mwaka wa fedha 2024/2025, Serikali imepanga kuanza ujenzi wa kilometa 11; kwa sehemu za Puge – Ndala kilometa tano; Ziba – Choma - kilometa mbili na Ziba – Nkinga kilometa nne. Kwa sasa kazi ya mapitio ya makabrasha ya zabuni inaendelea na mara baada ya kazi hiyo kukamilika zabuni zitatangazwa. Kwa sehemu iliyobaki, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara hiyo, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Gulamali.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri mwaka jana katika bajeti ilikuwa ya 2023/2024 tulitengewa kilometa kumi na mwaka huu wa fedha tulikuwa tumetengewa kilometa nyingine. Tulitarajia katika kutangaza zabuni kilometa zaidi ya 22 ziweze kutangazwa. Je, mtazingatia hilo Mheshimiwa Waziri? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema katika jibu langu kwamba tutaanza hizo kilometa 11, lakini kama hali ya bajeti tutapata fedha tutaendelea kuijenga na lengo si kujenga hii barabara tu kwa awamu, lakini tukiweza kupata hela nyingi zaidi tuna uwezo wa kuijenga hiyo barabara yote, lakini kwa sasa tutaanza na hizo kilometa 11, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Subira Mwaifunga.

Na. 151

**Serikali Kuuza Nyumba Zinazomilikiwa na *TBA***

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kuuza nyumba za *TBA* kama ilivyo kwa *NHC* ili ijiondoe kwenye biashara ambayo ina changamoto kwao?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imefanya mabadiliko Hati Idhini iliyoanzisha Wakala wa Majengo Tanzania *(TBA)* kupitia Tangazo la Serikali *(GN)* Na. 595 la tarehe 25 Agosti, 2023 ili kuwezesha Wakala kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa *TBA* imeanza kujenga nyumba za kuuza kwa umma wote kama ilivyo kwa Shirika la Nyumba la Taifa *(NHC)*. Tayari Wakala umeandaa orodha ya miradi ya ujenzi wa nyumba zitakazouzwa kwa wananchi wote.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hawa.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hizo nyumba ambazo wanataka kujenga na waanze

kuziuza, lakini *TBA* wana nyumba nyingi nchi nzima ambazo ni mbovu, zimechakaa na hawana uwezo wa kuzihudumia. *(Makofi)*

Je, Serikali ina mpango gani wa kuanza kuuza hizo nyumba ambazo mmezishindwa ili wananchi waweze kuzinunua na waweze kuzirekebisha? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili, kwa kuwa nyumba hizo hata hapa Dodoma zipo na baadhi ya Wabunge na wafanyakazi wengi wa Serikali wanaishi humo, je, huoni sababu ya ninyi kuanza kupita kwenye nyumba hizo na kuangalia hali mbaya iliyopo katika nyumba hizo? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema tumeshafanya mabadiliko ya Hati Idhini. Ilivyokuwa ilikuwa ni majengo ambayo yanajengwa kwa ajili ya watumishi wa umma, lakini kwa sasa baada ya kubadilisha tutajenga majengo ambayo sasa yatakuwa na uwezo wa kuuzwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu nyumba zilizochakaa, nataka tu nimkumbushe Mheshimiwa Mbunge kwamba kuna nyumba zilizokuwa za *TBA* lakini zipo nyumba zilizokuwa za TAMISEMI. Tulichofanya kama Wizara kupitia *TBA,* tayari wameshapitia nyumba zote ambazo zimechakaa na kuainisha mpango wa kuzikarabati na tayari tumeshaanza kukarabati nyumba hizo mikoa yote, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, nyumba kama za Mchikichini mmezichukuwa huu ni mwaka wa sita hamna chochote mnachokifanya, ni bora tu mzirudishe Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam.

Waheshimiwa tunaendelea, Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Maryam Azan.

Na. 152

**Uhifadhi wa Misitu Kutokana na Hewa ya Ukaa**

**MHE. MARYAM AZAN MWINYI** aliuliza: -

Je, Serikali ina mkakati gani wa kusimamia uhifadhi wa misitu ikizingatiwa kwamba imeandaa na kuzindua biashara ya hewa ya ukaa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania ina takribani hekta za misitu milioni 48.1 ambayo inajumuisha misitu ya Serikali Kuu, misitu ya halmashauri, misitu ya vijiji na misitu binafsi. Aidha, kutokana na kuongezeka kwa shughuli za kibinadamu kama kilimo cha kuhamahama, uchomaji moto kwenye misitu na ufugaji, nchi yetu inapoteza takribani hekta 469,000 kwa mwaka na hivyo kuchangia kuzalisha gesi joto na hatimaye uwepo wa mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, biashara ya kaboni ni mojawapo ya mkakati wa Kimataifa wa kusaidia kupata fedha za uhifadhi wa mazingira na misitu na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Kutokana na umuhimu huo, Serikali imeweka mikakati ya kulinda misitu iliyopo na kuongeza upandaji miti nchini. Serikali imefanya hivyo kupitia mikakati na miongozo mbalimbali ikiwemo Mkakati wa Kuongoa Misitu wa mwaka 2024, Makakati wa Mianzi wa mwaka 2024, Mwongozo wa Kitaifa wa Uandaaji na Utunzaji wa Kitalu cha Miche ya Miti wa mwaka 2024 pamoja na Mkakati wa Kitaifa wa Kilimo Mseto wa mwaka 2024. Hivyo, nitoe rai kwa wananchi kuendelea kuzingatia sheria za uhifadhi zilizowekwa na kutojishughulisha na shughuli za uharibifu wa misitu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Maryam.

**MHE. MARYAM AZAN MWINYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa wananchi wengi hawana uelewa wa biashara ya kaboni, je, Serikali ina mkakati gani wa kuimarisha biashara hiyo ya kaboni Tanzania Bara na Zanzibar?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kumekuwa na kampeni endelevu ya upandaji miti nchini, je, kampeni hii inakidhi utunzaji wa mazingira? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha kwamba elimu hii inatolewa, Ofisi ya Makamu wa Rais imekuwa na jukumu la kusimamia jambo hili na kwa mahsusi kabisa Kituo cha Taifa cha Uratibu wa Usimamizi wa biashara hii inafanya kazi kubwa ya kuwaelimisha wananchi na kama mnavyofahamu tayari Serikali ilitunga kanuni za usimamizi na udhibiti wa biashara ya kaboni ya mwaka 2022. Niwaombe wadau wetu wapate fursa ya kutembelea kwenye kituo chetu cha Taifa cha Uratibu na Usimamizi ili kupata taarifa za msingi za jinsi ya kuweza kushiriki kwenye biashara hii.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Waheshimiwa tunaendelea Wizara ya Mambo ya ndani Mheshimiwa Esther Matiko

Na. 153

**Ujenzi wa Vituo vya Polisi Wilaya za Kipolisi Tarime**

**MHE. ESTHER N. MATIKO** aliuliza: -

Je, lini Vituo vya Kipolisi Wilaya za Kipolisi Tarime, Sirari, Utegi na Nyamwaga vyenye hadhi kama Kituo cha Mtumba Dodoma vitajengwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inajenga kituo cha Polisi Daraja "A" Tarime ambacho kitagharimu kiasi cha fedha shilingi 1,200,000,000 na katika mwaka wa fedha 2024/2025 zimetengwa fedha kiasi cha shilingi 350,000,000 kuanza ujenzi huo. Aidha, Serikali itaviboresha Vituo vya Polisi Sirari, Utegi, na Nyamwaga ili viwe na hadhi ya Vituo vya Polisi vya Wilaya kwa kuweka mifumo na miundombinu ya kisasa ili kurahisisha utekelezaji wa kazi za polisi kwa mujibu wa matakwa ya haki jinai na kuzingatia mahitaji ya msingi ya makundi yote ya binadamu na tathmini kwa ajili ya utekelezaji huo umeshaanza kufanyika. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na naishukuru na Serikali *at last* imeanza ku-*take action* kwa kujenga hicho Kituo cha Tarime, lakini vituo vyote vya kipolisi ambavyo nimevianisha, Sirari, Utegi, Nyamwaga na Tarime ambacho mnaanza, kwa kweli vilikuwa havina hadhi kabisa, vina hadhi ya *out posts*. Kwa cha Tarime mmefanya, lakini hivyo vituo vingine nataka kujua badala ya kukarabati, ni kwa nini msiweke katika mpango mkakati ili muweze kuvijenga? Kwa sababu kusema mnaboresha miundombinu haina hadhi kabisa, walau cha Nyamwaga mnaweza mkashirikiana na wadau kama *TANAPA,* maana yake kile kituo kinahudumia sana Mbuga ya Serengeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, Kata ya Susuni na swali hili pia nimeuliza sana hapa, haina Kituo cha Polisi, lakini kata ya jirani ina vituo viwili vya Polisi, ambayo ni Kata ya Mwema, ina Kituo cha Kibuterere na kile ambacho kipo kwa Utambe, lakini wananchi wa Kata ya Susuni wanatembea zaidi ya kilometa 16

kutafuta huduma. Basi inaondoa na dhana kabisa ya ulinzi na usalama wa raia. Ni kwa nini Serikali msijenge Kituo cha Polisi katika Kata ya Susuni? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Esther Matiko, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza kwamba vile vituo vya Wilaya ambavyo amevieleza, ukiachia kile Kituo cha Tarime, tunaenda kuvifanyia marekebisho au ukarabati mkubwa ili viweze kukidhi mahitaji ya sasa hivi, lakini kuhusiana na Kituo hicho cha Susuni cha Kata ni miongoni mwa vituo vya kata ambavyo mwaka huu tutajenga, ambavyo katika Mkoa wa Mara peke yake tunajenga vituo vya kata 19. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Ndaisaba.

Na.154

**Vibali vya Msimu katika Ofisi za Uhamiaji**

**MHE. NDAISABA G. RUHORO** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa vibali vya misimu katika Ofisi za Uhamiaji ngazi za wilaya?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Sheria ya Uhamiaji Sura ya 54 Rejeo la 2016 ilifanya marekebisho ya Kanuni za Uhamiaji za mwaka 1997 kwa ajili ya kuzingatia haki ya kundi la wageni hasa kutoka nchi jirani wanaoingia nchini kufanya vibarua hususani katika sekta ya kilimo na nyinginezo za msimu. Kupitia

marekebisho hayo, Serikali ilianzisha aina maalumu ya kibali cha msimu yaani *Seasonal Migrant Pass* kupitia *GN* Na. 518 ya mwaka 2018 ambacho hutolewa kwa wageni hao kwa kipindi cha kuanzia miezi mitatu hadi sita ili kuendana na msimu wa kilimo. Kwa sasa Serikali imekamilisha ufungaji wa mfumo kwa ajili ya utoaji wa vibali hivyo katika ngazi ya mikoa na kwamba Serikali inaendelea na maandalizi ya kupeleka huduma hiyo katika ngazi ya wilaya kwa kuanzia na wilaya za mpakani.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ndaisaba.

**MHE. NDAISABA G. RUHORO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, wananchi wa mipakani wakiwemo wananchi wa Wilaya ya Ngara, baadhi wamekuwa wahanga…

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, tunaomba utulivu ndani ya Bunge.

**MHE. NDAISABA G. RUHORO:** Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wengi wa mipakani wakiwepo wananchi wa Wilaya ya Ngara wamekuwa wahanga wa maswahibu kadha wa kadha yanayowakuta kutokana na changamoto za kutofahamu sheria hii na taratibu hizi za vibali vya misimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni upi mkakati wa Serikali wa kupeleka elimu Ngara na maeneo mengine ya mipakani ili wananchi wajue taratibu za kupata vibali vya msimu kwa raia wa kigeni? Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na mkakati wa elimu, kwanza, tunaandaa utaratibu wa Uongozi wa Jeshi la Uhamiaji Tanzania na Jeshi la Uhamiaji la nchi jirani kwa upande wa mpakani mwa Jimbo la Mheshimiwa Mbunge, nadhani itakuwa ni nchi ya Burundi. Tunaamini kabisa Serikali za nchi husika zina wajibu na umuhimu mkubwa sana wa kuelimisha wananchi wao kutambua juu ya taratibu za kuweza kupata vibali hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano miongoni mwa changamoto ambazo zinakabiliana na utoaji wa vibali hivi ni wananchi kukosa elimu juu ya umuhimu au haja ya kuwa na hati za kusafiria katika nchi zao. Kwa hiyo, wengi walikuwa wakija wanakuwa hawana hati za kusafiria na hivyo kuleta usumbufu usiyokuwa wa lazima.

Kwa hiyo, jitihada hizo na mkakati huo umeshaandaliwa kati ya chombo cha uhamiaji cha nchi yetu na vyombo vya nchi jirani ili watusaidie kutoa elimu katika nchi yao, wakati Jeshi la Uhamiaji na Serikali kwa ujumla ikiendelea na jitihada zake za kutoka elimu kwa wananchi wa nchi yetu hasa wanaoishi katika maeneo ya mpakani.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, ahsante.

Katibu.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU WA BUNGE:**

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

**NDG. AZIZA WAZIRI KHEIR – KATIBU MEZANI:**

**Muswada wa Sheria ya Shirika la Utangazaji Tanzania wa Mwaka 2024**

*(Kusomwa Mara ya Kwanza)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Muswada huu naelekeza uende Kamati ya Miundombinu. Katibu.

**NDG. JOSHUA CHAMWELA, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 3) wa Mwaka 2024 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 3) Bill, 2024)***

*(Kusomwa Mara ya Kwanza)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Naelekeza Muswada huu uende Kamati ya Utawala, Katiba na Sheria.

Katibu.

**NDG. JOSHUA CHAMWELA, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

**TAARIFA YA KATIBU WA BUNGE**

**NAIBU SPIKA:** Taarifa ya Katibu wa Bunge.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 35(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 naomba kutoa taarifa kwamba Shughuli zote zilizokuwa zimewekwa kwenye Orodha ya Shughuli za Mkutano wa Kumi na Sita wa Bunge sasa zimemalizika.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

Katibu.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU WA BUNGE:**

**HOJA YA KUAHIRISHA BUNGE**

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri Mkuu, karibu. *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, shukurani, shukurani.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote ninaomba nitumie nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujalia afya njema na kutufikisha salama leo tunapoelekea kuhitimisha Shughuli za Mkutano wa Kumi na Sita wa Bunge la Kumi na Mbili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tuendelee kumuomba Mwenyezi Mungu atupe hekima na nguvu za kutekeleza majukumu yetu ya kila siku ili tuweze kuwatumikia wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Spika kwa kuendelea kuliongoza vyema Bunge Tukufu hususan huu Mkutano wa Kumi na Sita tutakaohitimisha hivi punde. Sina shaka, Waheshimiwa Wabunge wenzangu mtakubaliana nami kwamba Mheshimiwa Spika, ameendelea kuliongoza Bunge hili kwa busara na weledi wa hali juu, hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru wewe binafsi kwa kazi nzuri unayoifanya ya kumsaidia Mheshimiwa Spika kutekeleza majukumu ya kuliongoza Bunge. Vilevile niwashukuru Waheshimiwa Wenyeviti wa Bunge ambao ni Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, Mheshimiwa Joseph Kizito Mhagama na Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika kwa kazi nzuri wanayoifanya kukusaidia kuendesha Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawashukuru Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa maoni waliyoyatoa wakati wa kujadili miswada mbalimbali iliyowasilishwa wakati wa Mkutano huu. Maoni mliyoyatoa yana umuhimu mkubwa katika kusaidia Serikali kutekeleza mipango yake hususan kwenye utoaji wa huduma kwa wananchi.

Waheshimiwa Wabunge, napenda niwahakikishie kwamba Serikali ina thamini michango yenu, imeipokea na itaifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mtakumbuka katika hatua nyingine ya kuimarisha utendaji ndani ya Serikali, tarehe 14, Agosti 2024 Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alifanya mabadiliko madogo kwenye Baraza la Mawaziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na mabadiliko hayo kipekee nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu; pia Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Afya; Mheshimiwa Profesa Paramagamba John Aidan Mwaliko Kabudi

kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Katiba na Sheria; Mheshimiwa Balozi Dkt. Pindi Hazara Chana ambaye ameteuliwa kuwa Waziri wa Maliasili na Utalii. Vilevile Mheshimiwa Ridhiwani Jakaya Kikwete aliyeteuliwa kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Wenye Ulemavu; Mheshimiwa Deogratius Ndejembi kuwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, pamoja na Mheshimiwa Balozi Mahmoud Thabit Kombo aliyeteuliwa kuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niwapongeze Mheshimiwa Deus Clement Sangu, Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora; Mheshimiwa Cosato David Chumi, Naibu Waziri Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki anayeshughulikia Mambo ya Nje; Mheshimiwa Dennis Lazaro Londo, Mbunge, Naibu Waziri wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki anayeshughulikia Mambo ya Nje; na Mheshimiwa Hamza Johari ambaye ameteuliwa kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile kwa kuchaguliwa kuwa Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Afya Dunia, Kanda ya Afrika. Ushindi wa Dkt. Faustine Ndugulile umeakisi namna ambavyo nchi yetu imeendelea kuaminiwa kimataifa na jinsi tulivyoimarisha mahusiano ya kidiplomasia na mataifa mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima kubwa nitambue mchango mkubwa uliotolewa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa namna alivyotumia wigo wake katika kushawishi na kumwezesha Mheshimiwa Dkt. Ndugulile kupata kura nyingi za kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nawapongeza sana Waheshimiwa Mawaziri wawili walioshiriki mchakato huo, Mheshimiwa Jenista Mhagama - Mheshimiwa Waziri wa Afya pamoja na Mheshimiwa Thabiti Kombo - Mheshimiwa Waziri wa

Mambo ya Nje, ambao pia na wao wameshiriki kikamilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, nawapongeza Mheshimiwa Spika, ambaye kwa hakika tumeona manufaa ya nafasi yake ya kuwa Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani, kwani amefanya kazi kubwa ya kuhakikisha kwamba Dkt. Ndugulile anapokelewa na kuungwa mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nimalizie kwa kuipongeza timu aliyoiteua kwenda kuongoza kampeni za ushindi pale Congo Brazzaville, ikiongozwa na Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama pamoja na Mheshimiwa Elibariki Kingu, Mheshimiwa George Mwenisongole, Mheshimiwa Neema Lugangira na Mheshimiwa Shamsia Mtamba, Mbunge wa Viti Maalum. Hongereni sana kwa kazi nzuri iliyofanikisha nchi yetu kupata kiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na maazimio yaliyofikiwa katika Mkutano wa Kawaida wa 44 wa Wakuu wa Nchi na Serikali, uliofanyika tarehe 17 Agosti, 2024 Jijini Harare Zimbazwe, Tanzania imekabidhiwa nafasi ya Uenyekiti wa Asasi ya Ushirikiano katika Masuala ya Siasa, Ulinzi na Usalama *(SADC Organ and Politics, Defence and Security Troika)*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee kabisa naomba nitume nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Asasi hii wa *SADC Troika*. Hii ni heshima kubwa kwa nchi yetu. Ninampongeza sana Mheshimiwa Rais wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 15 Agosti, Jarida la *The African Times USA,* lilimtangaza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kuwa Rais bora Barani Afrika kwa mwaka 2023. Jarida hilo limevutiwa na jitihada za Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan za kuleta mabadiliko makubwa ambayo yameiinua Tanzania na kuing’arisha kwenye ukuaji wa uchumi, utawala bora na mageuzi ya kijamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jitihada zake za kukuza umoja, demokrasia na uwezeshaji wa wananchi, zimekuwa mfano wa kuigwa na viongozi mbalimbali Barani Afrika. Sisi sote ni mashuhuda kuwa Mheshimiwa Rais katika uongozi wake, amejenga miundombinu muhimu na mikubwa ikiwemo ya reli, viwanja vya ndege, mitambo ya kuzalisha umeme na barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nitambue mchango mkubwa uliotolewa na Mawaziri wetu katika kulifikisha Taifa letu kwa kutumia uzoefu wao kuhakikisha kuwa wanasaidia kufikasha jina na Dkt. Ndugulile kama nilivyotamka awali kupata kura nyingi za kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuwa mchoyo wa fadhila, nisipowashukuru Waheshimiwa Jenista Mhagama pamoja na Mheshimiwa Jaji Dkt. Elieza Mbuki Feleshi ambaye ameteuliwa kuwa Jaji wa Mahakama ya Rufani. Viongozi hawa nilifanya nao kazi kwa karibu na walinipa ushirikiano mkubwa na nitumie nafasi hii kuwashukuru sana na kuwatakia heri kwenye majukumu yao mapya waliyopewa. Ahsante sana Waheshimiwa Mawaziri na Mwanasheria Mkuu Mstaafu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nampongeza Mheshimiwa Dkt. Gladness Ladislaus Salema kwa kuchaguliwa kuiwakilisha nchi yetu kwenye Bunge la Afrika Mashariki. Tunamtakia heri anapokwenda kuiwakilisha nchi yetu kwenye medani za kikanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, licha ya teuzi za Mawaziri, Naibu Mawaziri na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Rais alifanya mabadiliko katika nyadhifa mbalimbali. Nitumie fursa hii kuwapongeza viongozi wote walioteuliwa kushika nyadhifa hizo na kuwatakia kila la heri katika kutekeleza majukumu yao mapya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii pia kuwapa pole Watanzania wote waliopatwa na majanga mbalimbali yaliyosababisha majeruhi, uharibifu wa mali na kuondokewa na

wapendwa wao. Kwa wale majeruhi, tuendelee kuwaombea kwa Mwenyezi Mungu aendelee kuimarisha afya zao ili waweze kuendelea na shughuli za uzalishaji mali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkutano huu wa Kumi na Sita wa Bunge umekuwa kielelezo muhimu wa mchango mkubwa wa Bunge letu Tukufu kwa nchi yetu. Sambamba na shughuli zingine zilizojitokeza katika Bunge hili lakini limetimiza wajibu wake mkubwa wa kutunga sheria kupitia miswada iliyowasilishwa na kujadiliwa na Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili, nakupongeza sana wewe pamoja na wasaidizi wako kwa usimamizi madhubuti na wa viwango wakati wa kujadili miswada hii muhimu kwa mustakabali wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba uniruhusu kueleza mambo kadhaa ambayo Bunge lako limeyatekeleza tangu Mkutano huu wa Bunge ulipoanza siku ya tarehe 27 Agosti, 2024 mpaka leo ambapo tunahitimisha rasmi Mkutano huu muhimu wa Kumi na Sita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mkutano huu wa Kumi na Sita wa Bunge, jumla ya maswali 154 ya msingi na mengine 459 ya nyongeza yaliulizwa na Waheshimiwa Wabunge na kujibiwa na Serikali. Pia jumla ya maswali nane ya papo kwa papo yalielekezwa kwa Waziri Mkuu na kujibiwa. Katika hatua hii Waheshimiwa Wabunge walijikita katika kuuliza maswali yaliyolenga kupata ufafanuzi wenye manufaa kwa ajili ya wananchi wanaowawakilisha na Taifa hili kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawapongeza sana Waheshimiwa Wabunge kwa kutekeleza kikamilifu jukumu lenu muhimu na kwa upande wa Serikali, maswali haya yameendelea kusaidia kufuatilia na kuchukua hatua katika masuala mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge lako Tukufu linao wajibu wa kupokea na kutoa taarifa zinazohusu matukio yaliyogusa Taifa

ambayo Bunge limeona haja ya kutolea maelezo. Hivyo, katika Bunge lako ziko taarifa za matukio zilizojadiliwa kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa ya kwanza ni Taarifa ya Mheshimiwa Spika kuhusu kumwapisha Mheshimiwa Balozi Mahmoud Thabit Kombo kuwa Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania baada ya kuteuliwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa ya pili ni Taarifa ya Mheshimiwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu miswada iliyopitishwa na Bunge na kwamba imeshasainiwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na imeshakuwa sheria na sheria hizo zinaanza kutumika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria ya kwanza ni Sheria ya Fedha na Matumizi, Sheria Na. 5 ya mwaka 2024 *(The Appropriation Act No. 5 of 2024)* na Sheria ya Fedha, Sheria Na. 6 ya mwaka 2024 *(The Finance Act No. 6 of 2024);* taarifa ya tatu ni Taarifa ya Kamati Maalum iliyoundwa kuchunguza mgogoro wa ardhi kati ya mwekezaji kwenye Shamba la Malonje na vijiji vinavyolizunguka shamba hilo, kikiwemo Kijiji cha Sikaungu katika Jimbo la Kwela na taarifa ya mwisho ilikuwa ni Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Bunge hili, Waheshimiwa Wabunge wamepata fursa ya kujadili miswada mbalimbali iliyoletwa Bungeni na kusomwa kwa mara ya pili na ya tatu na hivyo kuwezesha Bunge lako kutekeleza wajibu wake wa kutunga sheria. Katika Mkutano huu, Bunge lako Tukufu limepokea miswada ya sheria nane na kujadili, kisha kupitisha kama ifuatavyo: -

(i) Muswada wa kwanza ni Muswada wa Sheria ya Marekebisho Sheria ya Shule ya Sheria Tanzania ya Mwaka 2024 *(The Law School of Tanzania Amendment Bill 2024)*;

(ii) Muswada wa Sheria ya Viwanja vya Ndege Tanzania ya Mwaka 2024;

(iii) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Hifadhi ya Jamii ya Mwaka 2024 *(The Social Security Law Amendment Bill 2024);*

(iv) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria zinazohusu Ulinzi wa Watoto wa Mwaka 2024 *(The Child Protection Laws Miscellaneous Amendments Bill 2024);*

(v) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa ya Mwaka 2024 *(The Prevention and Combating of Corruption Amendment Bill 2024);*

(vi) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Ushindani wa Mwaka 2024 *(The Fair Competition Amendment Bill 2024);*

(vii) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2024 *(The Written Law (Miscellaneous Amendment) Bill 2024);* na

(viii) Muswada wa Sheria wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 2_ wa Mwaka 2024 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendment) (No. 2) Bill 2024)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge lako Tukufu limefanya kazi kubwa kwa weledi wa hali ya juu wakati wa kujadili miswada hii na kuwezesha utungaji wa sheria ambazo zimepitishwa na hatua zote. Wakati wa mjadala wa miswada hii tumeshuhudia Waheshimiwa Wabunge wakitoa maoni, ushauri na kufanya marekebisho ya sheria zilizopendekezwa katika miswada iliyowasilishwa. Hivyo nawapongeza sana Waheshimiwa Wabunge kwa mijadala yenu yenye tija na umakini iliyowezesha kutungwa kwa sheria hizi mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge lako Tukufu pia limepokea miswada miwili ya sheria ambayo ilisomwa kwa mara ya kwanza kama ifuatavyo:-

(i) Muswada wa Sheria Shirika la Utangazaji Tanzania wa Mwaka 2024; na

(ii) Muswada wa Sheria wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 3) wa Mwaka 2024 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendment) (No. 3) Bill 2024)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Maazimio ya Bunge yaliyotokana na Kamati iliyoundwa na Mheshimiwa Spika, katika Mkutano huu wa Bunge sambamba na shughuli nyingine Bunge lako Tukufu liliweka maazimio kufuatia taarifa iliyopokewa kupitia Kamati Maalum iliyoundwa kuchunguza mgogoro wa ardhi kati ya mwekezaji kwenye Shamba la Malonje na vijiji vinavyozunguka shamba hilo ikiwemo Kijiji cha Sikaungu katika Jimbo la Kwela. Maazimio yaliyofikiwa na Bunge ni:-

(i) Serikali ifuate taratibu ili ibatilishe umiliki wa shamba lote la Malonje, Shamba la Efatha pamoja na vitalu 51 kwa kuzingatia sheria na maslaki ya umma; na

(ii) Serikali iandae mpango wa matumizi bora ya ardhi katika vijiji vyote nane vinavyozunguka pamoja na Gereza za Mollo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa Serikali imeyapokea maazimio hayo ya Bunge na inayapa uzito mkubwa na hivyo tutaendelea na kuratibu namna bora ya kutekeleza maelekezo ya Bunge lako kupitia maazimio haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuzungumzia uchanguzi wa Mbunge wa Bunge la Afrika Mashariki. Kama mnavyokumbuka nchi yetu ilipata pigo la kuondokewa na mwakilishi wake Marehemu Mheshimiwa Dkt. Shogo Richard Mlozi

aliyekuwa Mbunge wa Bunge la Afrika Mashariki aliyefariki dunia tarehe 13 Juni, 2024 na kuzikwa tarehe 17 Juni, 2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Taifa tumepata pigo kubwa kulinganisha na mchango mkubwa uliotolewa na Mheshimiwa Dkt. Shogo Richard Mlozi katika kuyabeba maono ya nchi yetu na kuitetea kwenye Jumuiya yetu. Kufuatia kifo hicho nchi yetu ilipata pengo katika viti vya uwakilishi katika Bunge la Afrika Mashariki na hivyo kulazimika kufanya uchaguzi uliyofanywa kwa mchakato ndani ya vyama vya siasa na tarehe 5 Septemba, 2024 tumehitimisha kwa kufanya uchaguzi ambao umempata mshindi ambaye ni Mheshimiwa Dkt. Gladness Ladislaus Salema kuwa muwakilishi wetu kwenye Bunge la Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Dkt. Salema anaenda kuungana na Waheshimiwa Wabunge wenzake wanayoiwakilisha Tanzania katika Bunge hilo, hivyo kwa niaba ya Wabunge wenzangu na Serikali tunamtakia kila la kheri katika kuzisimamia na kuzipigania ajenda za Tanzania katika uwakilishi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuzungumzia mwenendo wa hali ya hewa nchini unaokwenda sambamba na msimu wa kilimo. Mamlaka ya Hali ya Hewa nchini imetoa utabiri wa mvua za vuli kwa kipindi cha mwezi Oktoba hadi Disemba, 2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa nchini mvua za vuli ni mahususi kwa maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua ambayo yanajumuisha Mikoa ya Kagera, Geita, Mwanza, Mara, Simiyu na Kaskazini mwa Mkoa wa Kigoma. Mikoa mingine ni Manyara, Arusha, Kilimanjaro, Tanga, Pwani, Dar es Salaam na Kaskazini mwa Mkoa wa Morogoro. Utabiri unaonesha kuwa mvua zitakuwa chini ya wastani hadi wastani katika maeneo mengine yanayopata mvua hizo na zinatarajiwa kuanza kwa kusuasua na kutawaliwa na vipindi virefu vya ukavu na mtawanyiko wa mvua usioridhisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, utabiri huu unaashiria kuwa shughuli za uzaliushaji wa mazao ya chakula zitaathirika hali inayoweza kupunguza utengamano wa upatikanaji wa chakula

katika maeneo yanayopata mvua hizo na maeneo mengine ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika msimu huu wa kilimo wa mwaka 2024/2025 Serikali itaendelea kutoa ruzuku ya mbolea kwa wakulima kama ilivyofanyika katika misimu iliyotangulia, aidha, kwa kutambiua mwenendo wa uzalishaji wa zao la mahindi na ongezeko la mahitaji yake ndani nan je ya nchi katika msimu wa 2024/2025 Serikali itatoa ruzuku ya mbegu bora za mahindi kwa wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee nitumie nafasi hii kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uamuzi wake wa kuendelea kutoa pembejeo muhimu kwa wakulima na hivyo kuchagiza maendeleo ya sekta ya kilimo kwa ajili ya manufaa ya wakulima na Taifa kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, uzalishaji wetu wa ndani wa mbolea na mbegu bora unaendelea kuimarika kutokana na jitihada zinazofanywa na Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi ambapo uzalishaji wa mbolea sasa umeongezeka kutoka tani 84,696 kwa mwaka 2022/2023 hadi kufikia tani 158,628 msimu wa 2023/2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha uzalishaji wa ndani wa mbegu zilizothibitishwa ubora za mazao mbalimbali nao umeongezeka kutoka tani 42,096 kwa msimu wa 2022/2023 hadi kufikia tani 56,114 msimu wa 2023/2024. Hali hii inaonesha kuimarika kwa ualishaji wa ndani wa pembejeo ikiwa ni hatua mahususi ya kuchangia utoshelevu wa pembejeo za kilimo ndani ya nchi. Kutokana na mwenendo wa mabadiliko ya hali ya hewa katika baadhi ya maeneo nchi yetu ni vyema tukachukua tahadhari mapema ili tuhakikishe tunazalisha mazao yanayokomaa kwa muda mfupi na kuwa na uhakika wa utoshelevu wa chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo basi nitumie fursa hii kuwahimiza wananchi kupanda aina ya mazao mbalimbali

yanayokomaa kwa muda mfupi na yanayostahimili ukame kwa upande mwingine Maafisa Ugani wawaelimishe wananchi wetu kuhusu mazao yanayopaswa kupandwa katika maeneo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uhifadhi wa chakula, Serikali kupitia Wakala wa Taifa Hifadhi ya Chakula inaendelea kununua ziada ya mavuno yaliyopatikana kutoka kwa wakulima kwa ajili ya kuyahifadhi. Sehemu ya hifadhi hiyo itatumika katika kuongeza upatikanaji wa chakula kwenye maeneo yatakayobainika kuwa na upungufu wa chakula hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nitoe wito kwa wananchi kutumia vizuri mavuno yaliyopatikana katika msimu wa kilimo wa mwaka 2023/2024 kwa kutunza chakula cha kutosha katika ngazi ya kaya kwa kuzingatia kanuni bora za uhifadhi mzuri wa mazao ya chakula. Nitumie nafasi hii kuwakumbusha wananchi kuendelea kutumia chakula kilichopo sasa kwa uangalifu mkubwa, kuhifadhi chakula cha kutosha katika ngazi ya familia na kuepuka matumizi mabaya ya chakula au yasiyokuwa ya lazima.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kusimamia ukusanyaji wa mapato ya nchi ambapo hali ya ukusanyaji wa mapato ya ndani kwenye Mamlaka ya Serikali za Mitaa katika kipindi cha mwezi Julai, 2024 imeendelea kuimarika. Jumla ya kiasi cha shilingi bilioni 113.701 imekusanywa sawa na 8% ya makisio ya mwaka 2024/2025 ya shilingi trilioni 1.356. Aidha, makusanyo halisi yameongezeka kutoka shilingi bilioni 90.665 yaliyokusanywa kipindi kama hiki cha Julai, 2023 ikiwa ni ongezeko la shilingi bilioni 23.036. Ongezeko la ukusanyaji wa mapato ya ndani katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa inachangiwa na mikakati mbalimbali inayoendelea kufanywa na Serikali ikiwemo usimamizi wa vyanzo vya mapato vilivyopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, zoezi la mara kwa mara la ufanyaji tathimini wa vyanzo vya mapato ndani ya halmashauri kwa halmashauri zote 184, kutoa elimu ya ulipaji ushuru na wananchi pamoja na kuendelea kusimamia matumizi sahihi ya Mfumo wa

*TAUSI* wa ukusanyaji mapato pamoja na mashine za kukusanyia mapato *POS*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuzungumzia miradi ya kimkakati nikianza na uzinduzi wa *SGR* – Dodoma. Katika mwaka wa fedha 2024/2025 Serikali itaendelea na jukumu la kuendeleza sekta ya uchukuzi ambapo pamoja na mambo mengine itasimamia na kuendeleza sekta ya reli ikiwemo ujenzi wa *SGR* na kuanza uendeshaji wa treni ya kisasa ya abiria kutoka Dar es Salaam hadi Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, itakumbukwa kuwa tarehe 31 Disemba, 2023 Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alielekeza kuanza uedeshaji wa reli ya *SGR* kwa kipande cha Dar es Salaam – Dodoma ifikapo mwezi Julai, 2024. Naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa safari za treni ya mwendokasi kutoka Dar es Salaam mpaka Morogoro zilishaanza tarehe 14 Juni, 2024 na tarehe 25 Julai, 2024 uendeshaji wa reli ya kisasa kutoka Dar es Salaam hadi Dodoma ulianza rasmi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, itakumbukwa tarehe 01 Agosti, 2024 Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alizinua utoaji wa huduma za reli ya kisasa *SGR* kutoka Jiji la Dar es Salaam kupitia Mkoa wa Morogoro hadi hapa Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, treni hiyo inaendelea kutoa huduma zake vizuri kwa wananchi na imechangia sana kuimarika sekta ya usafirishaji. Kipekee ninaomba kumpongeza sana yeye Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wetu kwa kusimamia maono yake na kwa kweli anahaidi, anatekeleza kazi iendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuzungumziea mapokezi ya ndege mpya *dream liner*. Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wake mahili Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeendelea kuboresha utendaji wa Kampuni ya Ndege Tanzania *(ATCL)* ili iweze kutoa huduma zenye

kuhimili ushindani katika soko la ndani kikanda na kimataifa kwa kuanzisha safari za moja kwa moja kuhudumia masoko hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha kuwa azma hiyo inatimizwa mnamo tarehe 20 Agosti, 2024 Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi aliipokea ndege kubwa mpya na ya kisasa ya masafa marefu aina ya *Boeng B787 – 8 Dream Liner* katika kiwanja cha ndege cha Kimataifa cha Sheik Abeid Aman Karume. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ndege hiyo ina uwezo wa kubeba abiria 262, kupokelewa kwa ndege hiyo kunaifanya *ATCL* kuwa na ndege 15 mpya ambazo zimenunuliwa kutokana na mpango wa ufufaji wa Shirika la Ndege la Tanzania ulioanza kutekelezwa 2016. Aidha, ndege hii mpya imeongeza fursa za ajira kwa marubani na wahudumu wa ndege. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ujio wa ndege hii ya kisasa umeiwezesha *ATCL* kuongeza miruko ya safari zake kwa vituo vya kikanda na kimataifa ambavyo vinahudumiwa kwa sasa pamoja na kuanzisha safari mpya katika vituo vya Kinshasa, Goma, Dubai, Muscat na Lagos. Kukua kwa mtandao wa safari za *ATCL* kunatokana na kuongezeka kwa ndege ambapo kutachangia kuongeza fursa za ajia kwa Watanzania na kuchagiza ongezeko la watalii kuja kutembelea vivutio mbalimbali hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie maandalizi ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa. Nchi yetu imekuwa na utaratibu wa kujenga misingi ya uongozi kuanzia ngazi ya chini ili kuwezesha Serikali kuwafikia watu wake katika kutekeleza masuala mbalimbali ili kufikia adhima kubwa katika kuleta maendeleo endelevu. Mwaka huu 2024 ni mwaka wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa katika nchi yetu, uchaguzi wa viongozi wa Serikali za Mitaa 2024 unatarajia kufanyika siku ya Jumatano 27 Novemba, 2024. Kazi za msingi zilizokamilika mpaka sasa ni pamoja na kuandaliwa kwa kanuni za uchaguzi wa viongozi wa Mamlaka za Serikali za

Mitaa, ngazi ya vijiji, vitongoji na mitaa katika mamlaka za wilaya na miji.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwongozo wa elimu ya mpiga kura na mwongozo wa uchaguzi wa Serikali za Mitaa unaendelea kutolewa. Maandalizi mengine ya uchaguzi yapo katika hatua za ukamilishaji ambayo yanajumuisha kutangaza orodha ya maeneo ya utawala, uhakiki wa vituo vya kupigia kura awamu ya pili na ununuzi ya vifaa vya uchaguzi. Kwa sasa mamlaka husika zinaendelea na utoaji wa elimu ya mpiga kura kupitia vyombo vya habari, mabango na mitandao ya kijamii. Kwa kuwa msingi wetu wa maendeleo unaanzia katika ngazi hii niwaombe Waheshimiwa Wabunge wenzangu kuhakikisha kwamba tunatumia fursa mikutano yetu tuwapo majimboni, wasanii na vyombo vya habari katika kutoa hamasa ya umuhimu wa wananchi kushiriki katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha niendelee kuwasisitiza Watanzania wote kuwa tayari na kutimiza haki yao ya Kikatiba kwa kuhakikisha wanashiriki kikamilifu katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwaka huu 2024. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie maandalizi ya Uchaguzi Mkuu 2025; Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi inaendelea na zoezi la uboreshaji wa daftari la kudumu la wapiga kura ikiwa ni sehemu ya maandalizi ya Uchaguzi Mkuu mwaka 2025. Kwa mujibu wa kifungu cha 16(5) cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani namba moja 2024 zoezi la uboreshaji wa daftari linatekelezwa katika awamu mbili, kati ya uchaguzi mkuu, moja uliyokamilika na siku moja kabla ya uteuzi wa mgombea wa Uchaguzi Mkuu unaofuata. Mtakumbuka tarehe 20 Julai, 2024 awamu ya kwanza ya zoezi la uboreshaji wa daftari la kudumu la wapiga kura ilizunduliwa Mkoani Kigoma, uzinduzi huo ulienda sambamba na kuanza kwa mzunguko wa kwanza wa uboreshaji wa daftari katika mikoa mitatu ya Kigoma, Tabora na Katavi. Zoezi hili linafanyika kwa siku saba kwa kila mkoa. Hadi sasa Tume imekamilisha zoezi la uboreshaji wa daftari katika mikoa saba ya Kigoma, Tabora, Katavi, Kagera, Geita, Mwanza na Shinyanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kuanzia tarehe 4 hadi tarehe 10 Septemba, 2024 uboreshaji wa daftari unaendelea katika Mikoa ya Mara, Simiyu na sehemu ya Mkoa wa Manyara katika Halmashauri za Wilaya ya Babati, Hanang, mbulu na Mji wa Babati. Zoezi hili linaendelea katika mikoa mingine kulingana na ratiba iliyopangwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa kifungu cha tisa cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani namba moja ya mwaka 2024 zoezi la uboreshaji wa daftari la kudumu la wapiga kura linahusisha Watazania wote wenye sifa za kuandikishwa wenye umri wa miaka 18 au zaidi na wale watakaotimiza umri huo wakati wa Uchaguzi Mkuu mwaka 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha uboreshaji wa daftari unatoa fursa kwa wapiga kura walioandikishwa na kwa bahati mbaya kadi zao zimepotea au kuharibika na wale ambao wamehama kutoka eneo moja la uchaguzi kwenda eneo lingine ama kuhamisha taarifa zao kufika vituoni ili kupata kadi mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwakumbusha wananchi wote kuwa zoezi hili halihusishi kubadilisha kadi za mpiga kura zenye jina la Tume ya Taifa ya Uchaguzi ili kupata kadi iliyoandikwa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi na kwa kuzingatia maboresho hayo niwatoe wasiwasi wananchi wote walioandikishwa mwaka 2015 na mwaka 2019/2020 kuwa kadi zao ni halali kwa mujibu wa kifungu cha 168 cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Namba 01 ya mwaka 2024 na zitatumika kwenye Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani mwaka 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaombe na kuwatia shime Waheshimiwa Wabunge kwanza kujitokeza kujiandikisha au kuboresha taarifa zenu, lakini mbili ni pamoja na kuwahamasisha wananchi wenye sifa za kuandikishwa katika majimbo yetu wajitokeze kwa wingi kujiandikisha au kuboresha taarifa zao pindi zoezi hili linapofanyika katika maeneo yao. Aidha, niwasisitize wadau wa ngazi ya Taifa, Mkoa, Halmashauri wahakikishe

wanavishirikisha vyama vya siasa katika zoezi hili kwa kuwa wao ni wadau muhimu sana katika masuala ya uchaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati naelekea kuhitimisha hotuba yangu nitumie fursa hii kutoa maelekezo yafuatayo:-

(i) Kwa Wizara ya Uchukuzi iendelee kusimamia kwa karibu Shirika la Reli ili kuhakikisha kwamba huduma za reli ya *SGR* zinazidi kuboreshwa na usimamizi wa miundombinu kuimarika na huduma bora ndani ya reli zitatolewa na kuhakikisha usalama wa abiria;

(ii) Wizara ya Kilimo isimamie kwa ukaribu upatikanaji na usambazaji wa pembejeo za kilimo hususani mbolea kwenye maeneo yote ikiwa ni sehemu ya maandalizi ya msimu ujao wa kilimo kwa kuzingatia jografia za kanda za kilimo nchini; na

(iii) Wizara ya Kilimo, Maafisa Ugani waendelee kutoa elimu kwa wakulima kuhusu matumizi ya teknolojia bora za uhifadhi wa mazao ya chakula na matumizi sahihi ya chakula na matumizi sahihi ya chakula katika ngazi ya familia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie kwa kuzungumzia sekta ya michezo; Ibara 243 ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM imeelekeza kuanzisha mipango na mikakati maalumu ya kuendeleza michezo ikiwemo uanzishaji wa shule maalumu za kukuza vipaji vya michezo *(sports academy)* ili waweze kukuza vipaji na kushindana katika soko la kimataifa. Hadi sasa zipo jumla ya *sports academy* 147 na vituo vya michezo 43 ambavyo vimewezesha kuibua na kuendeleza vipaji kwa vijana katika michezo ikiwemo mpira wa miguu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kwa sasa ujenzi wa kituo kikubwa na cha kimataifa cha *Suluhu Sports Academy* kinajengwa huko Kizimkazi, Zanzibar ambacho kinakuwa na viwanja vitatu vya soka vya kiwango cha kimataifa, majengo ya shule ya michezo, daharia kwa maana ya *hostel,* bweni kwa

maana ya *dormitory* na viwanja vya michezo mingine ikiwemo mpira wa kikapu, *netball,* wavu, mabwawa ya kuogelea, jengo la mazoezi, nyumba za walimu na wafanyakazi na msikiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe rai kwa Watanzania na kwa wadau wa michezo kuendelea kuanzisha vituo vya kukuza vipaji vya wanamichezo *(sports academy)* ili kuhakikisha vijana wanapata maandalizi, lakini pia kuibua vipaji na kuendeleza kwa lengo la kupata wachezaji kwenye vilabu mbalimbali kwa lengo la kutoa nafasi ya wachezaji wa ndani na hatimaye kuimarisha timu ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa jitihada za muda mrefu za Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo za kuimarisha timu za Taifa zinaanza kufikiwa, idadi ya wachezaji wa ndani kucheza mpira wa kulipwa inaongezeka hasa kwa mpira wa miguu na hasa kwa wanawake ukilinganisha na wanaume. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa takwimu za Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania zinasema timu ya Taifa ya Wanawake sasa inaweza kuundwa na wachezaji wa Kitanzania wanaocheza mchezo wa kulipwa nje ya nchi. Tunao wachezaji wanaofanya nje ya nchi vizuri ambao kwa sasa wana uwezo wa kuunda timu ya Taifa wakiwa wanatoka michezo ya kulipwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwatambue wachezaji wetu tuwatie moyo na pia kuwahamasisha wengine, wa kwanza ni Noela Patrick Luhala anacheza Israel, lakini Hasna Linus Ubamba yuko Egypt, Maimuna Musa Kaimu yuko Egypt, Suzan Adam Manumbu yuko Egypt, Akwila Sigaspar yuko Rwanda, Rehema Ramadhani anacheza Rwanda, Mariam Yusufu Juma anacheza Burundi, Julitha Singano anacheza Mexico, Opah Clement Tukumbuke yuko nchini China, Clara Cletus Luvanga yuko Saudi Arabia, Enekia Kisonga Lunyamila yuko Mexico, Diana Lucas Msemwa yuko Uturuki na Aisha Hamis Masaka yuko nchini Uingereza.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wachezaji hawa wanawake wamethibitisha kwamba inawezekana kucheza nje ya nchi mchezo wa mpira wa kulipwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapohitimisha hotuba yangu sasa nitumie nafasi hii kuwashukuru watendaji wote wa Serikali ambao wametumia weledi wao na kutoa michango ya kitaalamu na ushauri katika kufanikisha shughuli zilizopangwa kwenye Mkutano huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamshukuru sana Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kutekeleza wajibu wake ipasavyo hasa kuishauri Serikali vizuri katika kipindi chote cha Mkutano huu. *(Makofi)*

Pia namshukuru Katibu wetu wa Bunge na watumishi wote wa Bunge kwa kutupatia huduma nzuri iliyotuwezesha kutekeleza majukumu yetu ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee navishukuru vyombo vya ulinzi na usalama kwa kazi yao nzuri ya kuendelea kusimamia utulivu na amani katika kipindi chote kwenye viwanja hivi vya Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwashukuru sana waandishi wa habari kwa kazi nzuri mnayoifanya ya kuhabarisha umma juu ya yale ambayo yanajadiliwa na kufikiwa hapa Bungeni. Pia niwashukuru madereva wetu waliotuhudumia vizuri, wametuleta hapa, wametutembeza kipindi chote na tunaamini Mwenyezi Mungu atawaongoza kuturudisha makwetu vizuri. Tunawashukuru sana madereva wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwatakie Waheshimiwa Wabunge wenzangu safari njema na mnaporejea majimboni kwenu zaidi ya yote ninawaombea kwa Mwenyezi Mungu afya njema na ili mweze kuwahudumia wananchi katika majimbo yenu na maeneo ya uwakilishi mliopewa dhamana ya kuyaongoza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatarajia kwamba kati ya tarehe 15 au 16 Septemba, 2024 kutegemea mwandamo wa mwezi kutakuwa na Sikukuu ya Maulid. Nitumie nafasi hii kuwatakia heri waislam wote na watanzania kwa ujumla, maadhimisho mema ya mazazi ya Mtume Muhamad *(S.A.W)*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo sasa ninapenda kutoa hoja kuwa Bunge lako Tukufu liahirishwe hadi siku ya Jumanne, tarehe 29 Oktoba, 2024 saa 3.00 asubuhi litakapokutana tena katika ukumbi huu hapa Jijini Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono, Mheshimiwa Waziri Mkuu, nakushukuru sana. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa Iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**NAIBU SPIKA:** Katibu.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU WA BUNGE:** Wimbo wa Taifa na Wimbo wa Afrika Mashariki.

**NAIBU SPIKA:** Wimbo wa Taifa na Wimbo wa Afrika Mashariki.

**WIMBO WA TAIFA NA WIMBO WA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI**

*(Hapa Wimbo wa Taifa na Wimbo na Jumuiya ya Afrika Mashariki Ziliimbwa)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa Wabunge, wageni waliopo Bungeni asubuhi hii; wapo wageni wa Waheshimiwa Wabunge; wageni 70 wa Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, Naibu Waziri Mkuu na

Waziri wa Nishati pamoja na Mheshimiwa Saashisha Elinikyo Mafuwe, wahitimu wenzao wa Chuo Kikuu cha *St. Augustine* cha Jijini Mwanza, karibuni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wageni wa nne wa Mheshimiwa Paschal Katambi, Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu, wapiga kura wake kutoka Mkoa wa Shinyanga. *(Makofi)*

Wageni 23 wa Mheshimiwa Janeth Mahawanga, mabinti wajasiriamali kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; wageni 65 ambao ni waimbaji na Wachungaji kutoka Kanisa la Waadventista Wasabato Dodoma na Shinyanga. *(Makofi)*

Wageni wawili, Ndugu Gabriel Ndila na Ndugu Anna Mkoyi kutoka Ilazo, Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Bunge limehairishwa na nichukue nafasi hii kwanza kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, Serikali kwa ujumla, Mawaziri wote kwa utendaji uliotukuka na kufuata maelekezo yaliyotolewa na Mheshimiwa Rais, mmefanya kazi nzuri, hongereni sana. Niwapongeze Wabunge kwa kazi nzuri mliyofanya kipindi hiki chote ambacho tupo Bungeni. Mmeonesha umahiri wenu na mmeonesha mna sifa za kurudi tena Ubunge 2025. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, msiogope kwenda majimboni, niwaombe nendeni majimboni hiki sasa ni kipindi cha kwenda kuzungumzia faida ambayo tulipata kutokana na uongozi mahiri wa Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan. Kuna miradi ya kutosha ya kuzungumzia na juzi Mheshimiwa Rais kasaini mradi mwingine wa kuendeleza biashara na reli yetu ya *TAZARA*. Hiki ni kiwango kikubwa sana cha ufanisi wa diplomasia ya uchumi. Sasa mawe ya ngaka hakuna shida tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Gwajima, mawe sasa yanakuja na *TAZARA,* haya ndio maneno ya kwenda kusema jimboni msiogope. Msiogope Wajumbe, msiogope wagombea. Mnayo maneno ya kusema. Msirudi na unyonge, nendeni mkasifie Serikali ya Mama Samia. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, na neno la mwisho, ukiishi mbinguni, usiogope radi. *(Makofi/Kicheko)*

Naahirisha Shughuli za Bunge mpaka tarehe 29 Oktoba, 2024.

*(Saa 5.11 Asubuhi Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumanne, Tarehe 29 Oktoba, 2024 Saa Tatu Asubuhi)*